# Nipashe

Jumamosi Mei 29, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580595

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US





**UN** yaridhishwa na Samia utetezi wa haki za wanawake



UKURASA 3

**Bunge**, wanasheria waipa mbinu serikali mishahara ipande

UKURASA 4

UKURASA 11

# Mabilioni yachotwa wizarani kifisadi



• **Yamo** yaliyotumika kulipana posho ya bakshishi... *Ukurasa 2*

## YALIYOMO


**UKURASA WA 3**

**UFAFANUZI KUHUSU KILIMO CHA BANGI**

SERIKALI imesema haina mpango wa kuruhusu kilimo cha bangi...

**UKURASA WA 3**

**MWINYI ATUMIA BAISKELI KUSAKA WANAFUNZI KIJIJINI**

RAIS mstaafu wa awamu ya pili, Ali Hassan Mwinyi, amebainisha...

**UKURASA WA 7**

**KILIMO YAMULIKA MAENEO 7 MWAKANI**

WIZARA ya Kilimo imetaja vipaumbele saba vya kimkakati kwa...




Wananchi wakivuka kwa tahadhari daraja la mbao la Mto Mpiji, linalounganisha eneo la Mapinga, Kata ya Kiembeni, wilayani Bagamoyo, mkoani Pwani na Mbweni, mkoani Dar es Salaam jana. Wakazi wa maeneo hayo wameomba serikali kuwajengea daraja imara ili kurahisisha shughuli zao. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Mgambo matatani mauaji mume

UKURASA 2





Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store




# Polisi yaongeza kasi ujambazi, yaua Dar

UKURASA 2


**MICHEZO** **SIMBA, NAMUNGO HESABU HADHARANI** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Mabilioni yachotwa Hazina

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewasimamisha kazi Mkaguzi Mkuu, Mkaguzi Msaidizi na baadhi ya watendaji wa Wizara ya Fedha na Mipango ili kupisha uchunguzi wa tuhuma za matumizi mabaya ya fedha za umma zinazowakabili.

Vilevile, Majaliwa amemwagiza Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Kamishna wa Polisi Salum Hamduni, kufanya uchunguzi kuhusu tuhuma hizo na ikithibitika si za kweli, wahusika watarejeshwa kazini.

Watendaji hao wanadaiwa kuhusika na matumizi ya jumla ya Sh. bilioni 1.773 za wizara hiyo katika kipindi cha kuanzia mwishoni mwa Machi huu hadi mwezi huu.

Akizungumza katika kikao kazi cha viongozi wa wizara hiyo juzi, Majaliwa alizitaja baadhi ya tuhuma hizo kuwa ni malipo yaliyofanyika Machi 31, mwaka huu, kupitia vocha 30 ya Sh. milioni 251 yakielezwa kuwa ni malipo maalum bila kutaja kazi hiyo maalum ni ipi na nani aliifanya.

Pia, alisema siku hiyo ya Machi 31 zililipwa Sh. milioni 198.8 kwa madai kuwa ni posho ya honoraria. Alibainisha pia Aprili 8, mwaka huu, watumishi 27 wa wizara hiyo walilipwa Sh. milioni 44.5 zikiwa ni posho ya kazi maalum ya wiki nne.

"Pia Aprili 13, mwaka huu, zililipwa Sh. milioni 155.2 kwa watumishi 68 ikiwa ni posho ya kazi maalum ya wiki tatu, Aprili 30, mwaka huu zililipwa Sh. milioni 43.9 kwa ajili ya kuandaa mpango wa kuhifadhi mazingira na siku hiyo hiyo zililipwa Sh. milioni 14.4 kwa ajili ya Siku ya Wanawake.

"Fedha nyingine Sh. milioni 43 zililipwa siku hiyo na kufanya jumla ya malipo yaliyolipwa siku hiyo kuwa Sh. milioni 101.8," alisema.

Alisema kuwa Mei Mosi, mwaka huu asubuhi zililipwa Sh. milioni 184.1 na mchana zililipwa Sh. milioni 264 zikiwa ni malipo ya kazi maalum.

"Sisi tulikuwa Mwanza tunasherehekea Siku ya Wafanyakazi Duniani ninyi hapa ndani mnalipana posho.

"Mei 3, mwaka huu, zililipwa Sh. milioni 146.5 kwa watumishi 125 zikiwa ni malipo ya kuandaa Mpango Kazi wa Ununuzi, kazi ambayo ni sehemu ya majukumu yao ya kila siku na tarehe hiyo hiyo zililipwa Sh. milioni 171.2 kwa ajili ya kuandaa nyaraka za Bunge," alisema.

Majaliwa alisema Sh. milioni 155 zililipwa kwa baadhi ya watumishi zikiwa ni posho ya kuandaa miongozo ya kazi.

"Yaani hii kazi ya ukaguzi imelipwa kwenye maeneo manne, huu ni utaratibu wa wapi? Mnazidi kutupunguzia imani na sijaongelea eneo la kuhamisha mafungu na utaratibu kuhamisha fedha kisha mnakwenda kuzichukua huko mlikozihamishia," alisema.

Aliwataka watendaji wa wizara hiyo kujenga uaminifu kwa wanaokusanya mapato kwa kufanya kazi kwa uaminifu na alitahadharisha watakaoendelea kucheza na pesa za umma hatua kali zitachukuliwa dhidi yao.

Hayo yamejiri wakati uchunguzi wa vyombo vya dola ukiendelea kuhusu agizo la Rais Samia Suluhu Hassan wa madai ya kuchotwa kwa mabilioni Benki Kuu (BoT).

## Mgambo 4 mbaroni tuhuma za mauaji ugomvi wa mke, mume

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

MKAZI wa Kijiji cha Kumhasha Wilaya ya Kibondo mkoani Kigoma, anadaiwa kuuawa na askari wa Jeshi la Akiba (Mgambo) kwa kupigwa na fimbo ya chuma sehemu mbalimbali ya mwili wake.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kigoma, James Manyama, alisema mauaji hayo dhidi ya Liberatus Mkomed (40) yalitekelezwa Mei 23 majira ya usiku.

Kamanda Manyama alieleza siku hiyo kulitokea ugomvi kati ya Mkomed na mkewe, Scholastica Bakunda na wakati ugomvi huo ukiendelea, mgambo wanne waliingilia kati na kuanza kumshambulia Mkomed hadi kusababisha kifo chake.

Baada ya tukio hilo Mei 24, mwili wa Mkomed ulifanyiwa uchunguzi katika Hospitali ya Wilaya ya Kibondo kisha kukabidhiwa kwa ndugu kwa ajili ya taratibu za mazishi.

Alisema baada ya watuhumiwa kutekeleza mauaji hao, walikimbia kusikojulikana.

Manyama alisema jeshi hilo linawashikilia watuhumiwa hao kwa ajili ya uchunguzi zaidi, na kwamba baada ya taratibu kukamilika watafikishwa mahakamani.




Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, ACP Debora Magiligimba, akionyesha kwa waandishi wa habari jana, nyaraka za kughushi za Jeshi la Ulinzi la Wananchi Tanzania (JWTZ), zilizokuwa zikitumiwa na mtuhumiwa Dismond Zakaria (33) ambaye taaluma yake ni mwalimu na wenzake wawili kutapeli wananchi na kujipatia fedha kinyume na sheria, mkoani humo. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Polisi waongeza kasi ujambazi Dar es Salaam

**Na Maulid Mmbaga**

KATIKA kudhihirisha kuwa kasi ya mapambano dhidi ya ujambazi inaongezeka, Jeshi la Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam limesema limeua mtuhumiwa wa ujambazi Kilambo Obale (44), mkazi wa Chanika.

Imeelezwa kuwa mtuhumiwa huyo alikuwa katika jitihada za kukwepa askari baada ya kumtaka aonyeshe alipoficha silaha aliyokuwa akiitumia kufanyia uhalifu.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaa, Camillius Wambura, alisema Alhamisi saa tano usiku, mtuhumiwa huyo alikamatwa kwa makosa ya kujihusisha na matukio ya ujambazi katika mikoa ya Mara na Dar es Salaam.

Alisema baada ya mtuhumiwa huyo kuhojiwa, alikiri kujihusisha na matukio hayo na kumiliki silaha, hivyo askari walimwamuru kwenda kuonyesha silaha hiyo ilipo na walipofika eneo husika, alidai kuifukia ardhini na walipokuwa katika jitihada za kuitafuta, mtuhumiwa alikurupuka na kukimbia kuingia kwenye maporomoko ya kingo za bahari.

Alisema baada ya kujaribu kukimbia, askari walipiga risasi hewani ili kumwonya asimame, lakini hakutii na aliendelea kukimbia ndipo walimpiga risasi kwenye mguu wa kulia na kuanguka, na kwamba alifariki dunia wakati akiwahishwa katika Hospitali ya Mwananyamala.

"Baada ya tukio hilo askari waliendelea kuchimba eneo alioonyesha na kufanikiwa kuipata bunduki aina ya S/GUN yenye namba S/NO.006074010/CAR 00097133.

"Uchunguzi wa awali unaonyesha kuwa Aprili 23, mwaka huu mtuhumiwa huyo akiwa na washirika wake walivamia nyumbani kwa askari mstaafu wa JWTZ, Milton Lazaro, mkazi wa Masaki na kuiba vitu mbalimbali ikiwamo TV, laptop na fedha za Canada dola 2,700 pamoja na silaha hiyo," alisema.

Aliongeza kuwa Jeshi la Polisi pia linawashikilia watu 12 wanaohusishwa na tuhuma za uvunjaji nyumba usiku na kuiba ambao ni Tony Peter (25), mkazi wa Tandika; Omary Ally (32) (Mwananyamala); Karimu Ally (22) (Mbezi); Shaibu Saehe (18) (Goba) na Bahati Mahame (25), Msasani.

Wengine ni Hussein Ally (26), Mikocheni; Kimti Juma (22) Msasani; Abas Athumani (40) Mikocheni; Joseph Saimon (26) Msasani; Andrea Moses (25) Msasani; Shabani Omary (18) na Mohamed Seif (25) Goba, na kwamba wote walikuwa wakijihusisha na matukio ya uvunjaji na uporaji katika maeneo ya Mbweni, Mabwepande, Tegeta na Kawe.

"Watuhumiwa hao walikamatwa na walipopekuliwa walipatikana na vielelezo kama televisheni 13, simu 14, rejeta tatu, bampa moja la gari aina ya Marcedes Benz, kompyuta ya meza ni moja na mpakato tano, panga moja, jeki ya kuvunjia moja, kisu na Microwave. Mali hizo ziliibwa katika matukio mbalimbali katika maeneo hayo," alisema.

Aidha, alisema linawashikilia watuhumiwa saba kwa tuhuma za kujihusisha na uhalifu wa unyang'anyi majumbani, ambapo wamekuwa wakivizia wakazi wanaoishi maghorofa ya Karikoo wakati wa kazi bila hawapo majumbani na kuwaibia fedha na vitu vingine vya thamani.

Watuhumiwa hao ni Juma Athumani (35), mkazi wa Tandika,; Rajabu Bakari (25) Ukonga; Awadh Shaban (26) Ukonga; Betram Peter (25) Kimara na wengine watatu, ambao hawakutajwa majina yao.

"Jeshi la Polisi linaendelea na operesheni maalum ya kupambana na vitendo vya kihalifu katika maeneo yote ya Jiji la Dar es Salaam, hivyo tunatoa onyo kwa watu wote wanaopokea mali za wizi, waache mara moja kwani yeyote atakayekutwa na hatia hiyo, atachukuliwa hatua za kisheria," alisema Wambura.

## Mwinyi atumia baiskeli kusaka wanafunzi kijijini

**Na Christina Mwakangale**

RAIS mstaafu wa awamu ya pili, Ali Hassan Mwinyi, amebainisha alivyolazimika kuwa mbunifu na kutumia usafiri wa baiskeli kupita kila nyumba kijijini ili kupata wanafunzi kwa ajili ya shule aliyokuwa mwalimu mkuu wake.

Anasema aliamua kutembelea nyumba baada ya nyumba kijijini ili kushawishi na kuwapata vijana waliofikia umri wa kuanza shule.

Mwinyi anasimulia hayo kwenye kitabu chake cha 'Mzee Rukhsa, Safari ya Maisha Yangu', akisema kati ya matatizo aliyokumbana nayo akiwa mwalimu, ni idadi ndogo ya wanafunzi.

Anasema asubuhi aliutumia muda wake vizuri katika kufundisha na baadaye jioni kutumia usafiri wa baiskeli, akizingua kila kijiji kushawishi wazazi kuwaandikisha watoto wao shuleni.

"Asubuhi ninasomesha, jioni ninapanda baiskeli kuzunguka kijijini, nyumba kwa nyumba moja hadi nyingine, nilikuwa ninapokewa vizuri na wazazi.

"Mzazi mmoja alinieleza: 'Mwalimu umenipata, kukutatulia siwezi, kukubalia siwezi. Mimi mvuvi, mke wangu anashinda kwenye shamba, huyu kijana unayemtaka ndiye huenda kuchunga mbuzi.

"Labda nikupe huyu mtundu wa miaka 11, nilizunguka hivyo kufanya majadiliano na wazazi," anasimulia.


Mzee Mwinyi anasema ilimpasa kuendelea kufanya hivyo bila kukata tamaa hadi afikishe idadi ya watoto 45 kujaza darasa.

"Ufundisha wenyewe ulihitaji ubunifu mkubwa, maana hali ya madarasa, vifaa vya kufundisha, vilikuwa haba. Kwenye somo la Jiografia kwa mfano, tuliichora ardhini ramani moja ya Bara la Afrika na Zanzibar.

"Kabla yetu, walimu walikuwa wakilipwa vizuri sana. Lakini wakati wetu ndiyo tukakutana na vitimbi Bwana Forster (Mkurugenzi wa Elimu) aliyeweka mfumo wa mpya wa mishahara na kuipunguza sana," anasema Mwinyi ambaye wakati huo alikuwa Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Bumbwini.

Anasema kulikuwa na madaraja ya walimu kwa waliofikia sekondari, mishahara wao ulikuwa Sh. 90 kwa mwezi huku walioishia darasa la nane, wakilipwa Sh. 45.

Katika kitabu hicho ambacho, Hayati Benjamin Mkapa aliyeandika utangulizi, anamtaja Mwinyi kuwa kielelezo cha kiongozi aliyethubutu kuleta mabadiliko kiuchumi katika awamu ya pili.



Rais Samia Suluhu Hassan akiwa katika mazungumzo na Msaidizi wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN) na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia masuala ya Wanawake (UN Women), Dk. Phumzile Mlambo Ngcuka, Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## UN yaridhishwa na Samia kutetea haki za wanawake

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amekutana na kufanya mazungumzo na Msaidizi wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN) na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia masuala ya Wanawake (UN-Women), Dk. Phumzile Mlambo-Ngcuka.

Kwa mujibu wa taarifa ya Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais Ikulu, lengo la mazungumzo hayo yaliyofanyika Ikulu jana, ni kuendeleza ajenda zinazowahusu wanawake.

Dk. Phumzile alimshukuru Rais Samia kwa namna anavyounga mkono juhudi za kupigania masuala ya wanawake na ameahidi kuwa UN-Women itamuunga mkono katika juhudi hizo.

Amemualika kushiriki katika mkutano utakaojadili masuala ya kijinsia uliopangwa kufanyika Juni 30, mwaka huu Paris, Ufaransa, ambao madhumuni yake ni kuchagiza usawa wa kijinsia kama yalivyokubaliwa katika mkutano wa Beijing uliofanyika mwaka 1995 baada ya kuonekana baadhi ya maazimio yanasuasua.

Kuelekea mkutano huo nchi zitakazoshiriki zimegawanywa katika maeneo sita ya kufanyia kazi na Rais Samia amekubali kuwa kiongozi katika eneo la haki za kiuchumi.

Aidha, Dk. Phumzile ameeleza kufurahishwa kwake na sekta binafsi ya Tanzania ambayo imekubali kushirikiana na serikali kusaidia juhudi za kuleta usawa wa kijinsia katika masuala ya kiuchumi kwa wanawake.

Kwa upande wake, Rais Samia ameipongeza UN-Women kwa juhudi kubwa za kupigania masuala ya wanawake ikiwamo maazimio ya Beijing na ameeleza kuwa Tanzania ipo tayari kuungana na UN-Women katika kuongeza msukumo wa utekelezaji wake.

Alibainisha kuwa japo Tanzania bado haijafikia kiwango cha usawa wa kijinsia cha 50/50 katika uongozi, katika kipindi chake atahakikisha anaongeza jitihada za kufikia usawa huo.

Rais Samia aliishukuru UN-Women kwa utayari wake wa kuisaidia Tanzania katika kukabiliana na janga la ugonjwa wa Covid-19.

## Ufafanuzi kilimo cha bangi

SERIKALI imesema haina mpango wa kuruhusu kilimo cha bangi nchini kwa kuwa bidhaa hiyo ni miongoni mwa dawa za kulevya.

Juzi, Nipashe ilimnukuu Kaimu Kamishna Kitengo cha Huduma za Sheria wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Christina Rwehabuza, akibainisha kuwa wamefanya marekebisho ya kifungu cha 12 ili kuruhusu kilimo cha bangi kutumika katika masuala ya tiba na utafiti.

Hata hivyo, uongozi wa juu wa mamlaka hiyo ulisisitiza juzi kuwa kamwe Tanzania haitaruhusu kilimo cha bangi, kwa kuwa ni haramu na kwamba nchi inayo mazao mengi ya biashara yanayotosha kuiingizia mapato.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini katika mamlaka hiyo, Florence Khambi, nchi haijaruhusu kilimo cha zao la bangi kutokana na madhara mbalimbali yanayotokana na matumizi yake.

"Ikumbukwe kuwa taarifa inayosambaa ikieleza kuwa Umoja wa Mataifa (UN) umeruhusu kilimo cha bangi kwa matumizi ya binadamu siyo sahihi, isipokuwa umoja huo umerekebisha baadhi ya vipengele vya udhibiti wa bangi pamoja na mawazo yake ili nchi nyingi ziridhie bangi itumike katika utafiti na kutengeneza dawa za tiba," alisema katika taarifa yake hiyo.

Mamlaka hiyo ilibainisha UN inasisitiza bangi itaendelea kuwa dawa za kulevya inayodhibitiwa kimataifa.

**Mhariri**




RIPOTI MAALUM-2

# Ijue siri mishahara watumishi wa umma kutopandishwa miaka sita

## ●Bunge, wanasheria waipa mbinu serikali kuepuka athari hasi kiutendaji

Na Sanula Athanas

**KATIKA sehemu ya kwanza ya ripoti hii jana, ulitolewa ufafanuzi wa kina kuhusu sababu za kiuchumi na kisheria zilizochangia uamuzi wa serikali wa kutopandisha mishahara ya watumishi wa umma kwa miaka sita mfululizo.**

**Vilevile, Rais mstaafu wa awamu ya pili, Ali Hassan Mwinyi, akaweka bayana kwamba tatizo hilo ni la kihistoria, akibainisha lilianza mwaka 1980 wakati wa uongozi wa Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere. Endelea na sehemu ya pili kujua undani wa mustakabali wake.**

-----------------------------------------------

ILI kutimiza ndoto za watumishi wa umma za kuongezwa kwa ujira wao, Mbunge wa Viti Maalum, Halima Mdee (CHADEMA), anaishauri serikali kuruhusu taasisi za nje ya nchi kuja kufanya tathmini ya kifedha (credit rating).

Mdee ambaye katika Bunge la 11 alikuwa Waziri Kivuli wa Fedha na Mipango, anasisitiza kuwa kwa kuruhusu taasisi huru kufanya tathmini ya kifedha nchini, kutaisadia Tanzania kupata mikopo yenye riba nafuu badala ya mikopo ya kibiashara yenye masharti magumu inayopewa sasa.

Anasema uamuzi huo utaleta ahueni kwenye Deni la Taifa ambalo ni sehemu ya mzizi mkuu wa kutopandishwa kwa mishahara ya watumishi wa umma.

"Kwa hali ilivyo sasa, ninaona kuna haja kuruhusu taasisi huru zije kutufanyia 'credit rating' ili kutusaidia kama taifa kujua deni letu halisi likoje.

"Kwa kutofanyiwa 'credit rating', benki nyingi za kimataifa zenye mikopo ya riba nafuu zitaendelea kutuogopa kutukopesha kwa sababu hazina uhakika kama tutalipa au la. Matokeo yake tutaendelea kukopa kwa masharti magumu ya kibiashara," Mdee anashauri.

Mbunge huyo ambaye kitaaluma ni mwanasheria, pia ana ushauri kwa serikali kufanya marekebisho katika Sheria ya Deni la Taifa ambayo ina miaka zaidi ya miaka 40 tangu kutungwa kwake.

Anapendekeza marekebisho ya sheria yalenge kukabiliana na kupaa kwa Deni la Taifa kwa kuitaka serikali kuwa makini katika ukopaji mpya, akisisitiza inapaswa kukopa kutekeleza miradi ambayo ina uhakika itarejesha fedha.



Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba.



Mbunge wa Viti Maalum, Halima Mdee (CHADEMA).

**HALI YA DENI LA TAIFA**

"Sheria yenyewe ya Deni la Taifa imepitwa na wakati. Ni sheria ya miaka ya 1970. Hoja hapa ni kwamba tuwe na sheria inayoitaka serikali kukopa pale tu inapohitaji kutekeleza miradi yenye uhakika wa kurejesha fedha na kulipa deni," Mdee anasema.

Februari 8, mwaka huu, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Sillo Baran, aliliarifu Bunge kuwa hadi Desemba mwaka jana, Deni la Taifa lilikuwa limefikia Sh. trilioni 59 kutoka Sh. trilioni 54.8 Desemba 2019, sawa na ongezeko la asilimia 7.6.

Baran alifafanua kuwa deni la ndani ni Sh. trilioni 16.2 na deni la nje ni Sh. 42.8 na kwamba ongezeko hilo limesababishwa na mikopo mipya ambayo serikali imeichukua ili kugharamia miradi ya maendeleo.

"Kamati inaishauri serikali kukamilisha haraka mchakato wa nchi yetu kufanyiwa 'credit rating' ili kuiwezesha serikali kupata mikopo nafuu na kwa urahisi," Baran alisema.

Nipashe inatua mezani kwa Dk. Mwajuma Kadilu, Mkuu wa Idara ya Sheria za Madai na Jinai katika Kitivo cha Sheria cha Chuo Kikuu cha Mzumbe, ambaye anaishauri serikali kupandisha mishahara ya watumishi wa umma ili kukidhi matakwa ya kisheria.

Dk. Mwajuma ana ufafanuzi zaidi katika hili akisema: "Sheria za kazi tunazozitumia sasa zilitungwa mwaka 2004 na zinataka kila baada ya miaka mitatu mabadiliko ya ujira, kukielekezwa viwango tofauti vya mishahara kulingana na sekta na skimu za utumishi.

"Mwaka 2007 tukawa na mabadiliko katika ujira wa watumishi, mwaka 2010 tukawa na mabadiliko na mengine yalishuhudiwa mwaka 2013 ambayo ndiyo 'wage order' inayotumika hadi sasa.

"Kwa maoni yangu, hii imepitwa na wakati. Kwa mfano, inasema kima cha chini cha mshahara wa 'house girl' (msichana wa kazi za nyumbani) unayeishi naye na anayekutegemea kwa chakula, malazi, matibabu na mengineyo, uwe Sh. 40,000 na kama anakuja na kuondoka umlipe Sh. 60,000.

"Kwa gharama halisi za maisha, viwango hivyo ni vidogo mno. Kwanini hatukuwa na viwango vipya vya mishahara mwaka 2017 na 2020 kama sheria inavyotaka?

"Je, ni Labour, Social and Economic Council haikutimiza wajibu wake au bodi za mishahara? Ni mawaziri wa kazi na yule wa utumishi wa umma wametukwamisha? Kuna sababu nyingine tofauti na hii ya hali ya uchumi wa nchi?" Dk. Mwajuma anahoji.

Kwa mujibu wa TUCTA, tangu mwaka 2014, watumishi wa umma nchini hawajashuhudia ongezeko katika ujira wao wa kila mwezi.

HABARI KITAIFA

# Wabunge wataka kanuni uvuvi zipitiwe



**Na Salome Kitomari,** DODOMA

WABUNGE wameitaka serikali kupitia upya sheria na kanuni zinazosimamia mifugo na uvuvi, wakisisitiza zimekuwa kandamizi dhidi ya ukuaji endelevu wa sekta hizo.

Pia wametaka ushirikishwaji wa karibu wa wadau wa sekta hiyo kwenye mabadiliko ili kuondoa malalamiko na kuwa na sheria halisi.

Wakichangia mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi bungeni juzi, wabunge hao walisema bila kufanya hivyo, malalamiko katika sekta hiyo hayataisha na itaendelea kudumaa.

Mbunge wa Buchosa (CCM), Erick Shigongo, (pichani) alisema nchi imekosa utashi wa kisiasa katika sekta hizo kiasi cha kushindwa kubadilisha maisha ya watu.

"Nimesoma sheria ya Uganda na Tanzania, ya kwetu iko kwa ajili ya kudhibiti na wenzetu ni kwa ajili ya kuwezesha, tukiendelea hivi tutabaki kukamata nyavu za wavuvi, kuzichoma bila mafanikio, inatakiwa nguvu iwe kwenye kuwezesha," alisema.

Kwa majibu wa Shigongo, Uganda ina Ziwa Victoria kwa asilimia 45 na uvuvi unachangia asilimia tisa ya Pato la Taifa, huku Tanzania yenye eneo kubwa, uvuvi ukichangia asilimia 12.

Alisema samaki anatoa protini ya asilimia 20 huku Uganda ikiwa ni asilimia 50, huku ulaji wa samaki nchini humo mtu mmoja anakula kilo 15 hadi 20 na Tanzania ni kilo 5.5, kiwango ambacho ni kidogo.

Mbunge wa Ole, Omari Issa Kambo, alisema sheria na kanuni zilizopo hazimsaidii mvuvi bali zinamkandamiza kwa kisingizio cha uvuvi haramu na uharibifu wa mazingira.

"Lini sheria na kanuni zetu zitafanyiwa mabadiliko ziendane na hali za watu wetu? Kuwaambia wavue mita 50 huku wana zana duni mwisho watafariki dunia na tutabaki na yatima na wajane wengi," alisema.

Mbunge wa Mbogwe (CCM), Nichodema Maganga, alisema sheria ni kandamizi na zimekuja kwa ajili ya kuwaumiza wafugaji na wavuvi kiasi cha kuiacha sekta nyuma.

Akijibu hoja hizo, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, alisema wadau watashirikishwa wakati wa mapitio ya sheria hizo na kwamba matumizi ya taa katika uvuvi yalizingatia utafiti wa kitaalamu.

## Serikali yafanya tathmini NARCO

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

SERIKALI imesema inafanya tathmini ya kina ya Shirika la Ranchi za Taifa (NARCO), ili kuona kama malengo ya uanzishwaji wake yamefikiwa na nini kifanyike katika kubadilisha ili kuwe na tija.

Akijibu hoja mbalimbali za wabunge zilizotokana na hotuba ya mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Waziri Mashimba Ndaki, alisema jitihada mbalimbali zimefanyika ikiwamo kukodisha asilimia 75 ya eneo na kubakiwa na asilimia 25, lakini bado hakuna matokeo chanya.

"Tunaomba mtupe muda ili tuje na mkakati, wataalamu wetu wafanye tathmini, utendaji wake, malengo ya uanzishwaji wake na kuona namna yanavyoweza kuleta tija, namna yanavyoenda haujafikia tija ambayo wananchi walikuwa wanategemea.

"Tumejitahidi kuja na mkakati wa kukodisha kwa asilimia 75 na asilimia 25 imebaki NARCO, lakini hakuna tija na ndiyo maana tunaomba tufanye tathmini ili kutatua hili tatizo," alisema.

Waziri alilazimika kutoa ufafanuzi huo baada ya Mbunge wa Muleba Kaskazini (CCM), Charles Mwijage, kusema ni muhimu Bunge likajadili na kuazimia kufutwa kwa NARCO kwa kuwa hadi sasa imeshindwa kutekeleza wajibu wake na kufikia malengo ya uanzishwaji wake.

Mwijage pia alishika shilingi ya mshahara wa waziri na kuomba Bunge lijadili suala hilo.

## Maboresho ya reli ya TAZARA yakwamba

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MAZUNGUMZO ya kuboresha reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) yamekwama kuendelea, kutokana na mchakato wa uchaguzi mkuu unaoendelea Zambia.

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, anayeshughulikia Uchukuzi, Mwita Waitara, aliyasema hayo jana alipotembelea karakana ya kukarabati vichwa vya treni Iyunga jijini Mbeya.

Alisema kwa sasa reli hiyo inahitaji kufanyiwa maboresho makubwa, lakini kutokana na sheria inayounda Shirika hilo, Serikali ya Tanzania haiwezi kutekeleza maboresho hayo mpaka ifikie makubaliano na Serikali ya Zambia.

"Reli hii inahitaji kufanyiwa maboresho makubwa, lakini kama mjuavyo reli hii inamilikiwa na TAZARA ambalo kisheria linamilikiwa na nchi mbili za Tanzania na Zambia, kutokana na sheria hiyo sisi Watanzania hatuwezi kufanya maboresho hayo mpaka tukubaliane na wenzetu wa Zambia," alisema na kuongeza:

"Tulishaanza mazungumzo ya kulifanyia shirika hili maboresho yanayohitajika, lakini kabla hatufikia makubaliano, wenzetu wa Zambia wakaingia kwenye mchakato wa uchaguzi, hivyo mazungumzo yetu yakasimama, hivi sasa tunawasubiri wamalize uchaguzi ili apatikane Waziri wa Uchukuzi kwa upande wao ndipo tukamilishe mazungumzo yetu."



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Udhamini mpya Ligi Kuu Bara uongeze ushindani

**WAKATI** Ligi Kuu Bara msimu huu wa 2020/21 unaelekea ukingoni na kila timu ikipambana ili kufikia malengo yake, Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), limeingia mkataba mpya wa udhamini wa miaka 10 na Kampuni ya Azam Media kwa ajili ya uendeshaji wa ligi hiyo ya juu nchini.

Mkataba ambao TFF imeingia na kampuni hiyo ambayo imepata haki ya kuonyesha mubashara mechi zote za Ligi Kuu Tanzania Bara una thamani ya Sh. bilioni 225.6.

Nipashe tunasema historia imeandikwa au ndoto za kufikia mafanikio zinaelekea kutimia kwa kuangalia udhamini huo ambao kwa kila msimu zitatumika Sh. bilioni 12, wakati udhamini uliomalizika ulikuwa ni wa Sh. bilioni nne kwa msimu.

Jambo kubwa na la kupongezwa, kiasi kikubwa cha fedha kitakachotolewa na wadhamini hao yaani zaidi ya asilimia 60, kitakwenda moja kwa moja kwa timu ambazo ndio wadau wakuu wa ligi hiyo inayotoa mwakilishi wa Tanzania Bara kwenye mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Kiasi kingine kilichobakia kitapelekwa katika majukumu mengine ya kiutawala, lakini yanayohusiana na ligi hiyo ambayo kuanzia msimu ujao itashirikisha timu 16 tu.

Katika kuonyesha Azam Media wanahitaji kuona Ligi Kuu Tanzania Bara itakuwa yenye ubora na itakayotoa matunda mazuri, imeahidi kusimamia matumizi ya fedha zitakazokuwa zinatolewa kwa timu zote zinazoshiriki pamoja na wasimamizi wa mpira huo ambao ni TFF.

Lengo la kusimamia matumizi ambayo yatatolewa kwa mfumo wa kielektroniki ili kufahamu wakati fedha hizo zinapotoka na kufuatilia matumizi yake ambayo yameainishwa kwenye makubaliano rasmi yaliyosainiwa na mabosi wa pande zote mbili.

Wadhamini hao wameamua kufuatilia matumizi ya fedha wanayowekeza kwa sababu wanahitaji kuona matunda yake na si kunufaisha viongozi au waajiriwa wengine ambao hawajakusudiwa katika makubaliano rasmi ambayo yalipelekea mabilioni hayo yatolewe.

Ili udhamini huo uonekane kuwa na faida, huu ni wakati kwa viongozi wa timu kuonyesha weledi kwa vitendo ili kutowakera mabosi hao walioamua kuweka historia ya kumwaga kiasi kikubwa cha fedha kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Viongozi wa timu wanatakiwa kusimamia vyema mchakato wa usajili wa wachezaji na makocha wenye uwezo ambao wataunda benchi la ufundi lililokamilika na kamwe kuacha kuwekana kwa kuzingatia 'uswahiba' ambao mwisho wa siku hushindwa kuonyesha uwezo katika kuiongoza klabu husika.

Wadau wote muhimu wa soka wanatakiwa kuutendea haki udhamini huu uliopatikana kwa kuhakikisha wanaziandaa timu zao mapema na hatimaye kupelekea ushindani zaidi katika msimu ujao, na kwa hali hiyo tutarajie kuwa na kikosi imara cha Timu ya Taifa (Taifa Stars), ambacho huundwa na idadi kubwa ya wachezaji wanaoshiriki ligi hiyo.

Tunatarajia kwa kiasi kikubwa cha bonus kilichotangazwa kwa timu zitakazofanya vizuri, timu zote zitaonyesha ushindani kuanzia mechi ya kwanza hadi ya mwisho kwa sababu ya kuhitaji kuondoka na fedha itakayokwenda kuwasaidia kujiimarisha kabla ya kuanza kwa msimu mpya.

Wakati umefika kwa kila timu kuacha kufikiria kushiriki na badala yake kuonyesha ushindani na mwisho wa msimu, timu itavuna kiasi cha fedha kulingana na namna ilivyopambana na si hali ilivyo sasa baadhi ya timu kujiona wao ni wasindikizaji na si wanaostahili kutwaa taji la ubingwa.

Mpira ni pesa, kauli hii ionekane kwa vitendo kwa klabu kupambana kuwania donge nono la Sh. milioni 500 ambalo litatolewa kwa misimu mitatu mfululizo kwa timu itakayonyakua ufalme huku kiasi kingine cha zawadi kikitofautiana kulingana na nafasi ambayo timu husika itamaliza.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Barnabas Maro

## Muungwana Lazima Nilonge

# Mdharau biu hubiuka yeye

**MTU** anayemdharau kilema huweza kujilaani mwenyewe. Methali hii yatufunza tusiwe na tabia ya kuwadharau watu wenye vilema au kasoro fulani za kimaumbile.

Wakati wawakilishi wa Tanzania, Simba walipokuwa wakijiandaa kupambana na Kaizer Chiefs nyumbani kwao (Afrika Kusini), baadhi ya magazeti ya michezo humu nchini yaliandika kwa kirefu Mnyama angeishinda timu hiyo kutokana na kuwakosa baadhi ya wachezaji wao maarufu ambao walikuwa majeruhi.

Ikaelezwa pia Kaizer Chiefs haipo kwenye nafasi nzuri kwenye msimamo wa ligi ya kwao, hivyo ni rahisi Simba kuwafunga huko huko kwao.

Kwa hiyo Simba ilikwenda Afrika Kusini ikiamini kabisa kuwa itaishinda Kaizer Chiefs na kufanya mchezo wa marudiano nyumbani jijini Dar es Salaam kumaliza kazi kwani utakuwa rahisi zaidi. Tegemeo la Simba halikuwa hivyo kwani mshangao wao na baadhi ya Watanzania, wakafungwa mabao 4-0 ugenini; Lahaula! (tamko linalotumiwa na mtu anapotanabahi baada ya kusahau au kushtukia jambo).

Kumbe "Mla cha mwenziwe na chake huliwa." Ndivyo ilivyokuwa kwa Kaizer Chiefs ilipokuja Tanzania kurudiana na Simba, hawakujua Simba walikuwa na ghadhabu dhidi yao, kwani walijiandaa ipasavyo wakisema kama walifungwa ugenini kwa nini nao wasishinde nyumbani kama walivyofanya wenyeji wao?

Mchezo waliocheza Simba kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam uliwashangaza wengi, baadhi yao wakiuliza: "Kwa nini hawakucheza hivyo kule Afrika Kusini?" Pengine waliwadharau wenyeji wao baada ya kusikia matatizo ya baadhi ya wachezaji walioumia hivyo wenyeji walijitahidi vilivyo hata mwisho wa mchezo wakiwa wamefunga mabao 4-0 na kuifanya Simba irudi nyumbani kwa masikitiko, wakiwa na lao.

"Kimya kingi kina mshindo mkuu." Mtu ambaye ni mnyamavu kwa muda mrefu huweza kuwa hatari anapokasirika. Hutufunza tusiwe na tabia ya kuwabeza au kuwadharau watu wanyamavu. Siku Simba walipoingia dimbani kwa Mkapa walikusudia kulipa kisasi kwa lengo la kupindua meza, lakini waliangushwa na mchezaji wao aliyeshindwa kufunga mabao matatu ya wazi!

**Alikuwa na kiwewe cha nini? "kiwewe" ni wasiwasi unaomwingia mtu; hali ya kuchanganyikiwa au kutojua la kufanya kutokana na kupatwa na hofu kubwa; babaika, wasiwasi. Kilichomfanya ababaike na kuwa na wasiwasi ni kitu gani?**

Alikuwa na kiwewe cha nini? "kiwewe" ni wasiwasi unaomwingia mtu; hali ya kuchanganyikiwa au kutojua la kufanya kutokana na kupatwa na hofu kubwa; babaika, wasiwasi. Kilichomfanya ababaike na kuwa na wasiwasi ni kitu gani?

Matokeo yake, Simba walitoka uwanjani kwa ushindi wa mabao 3-0 badala ya kusawazisha mabao 4-0 waliyofungwa ugenini ambayo yangesababisha kupigiana penalti. Kama Simba ingeshinda kwa mabao 5-4 ingeendelea na huenda ingetwaa kombe hilo la Afrika kwa mara ya kwanza sio Tanzania tu, bali nchi zote za Afrika Mashariki na majirani wengine.

Nawaambia Simba kuwa "Bahati ina miujiza lakini haina ahadi." Maana yake kwa kawaida bahati huweza kuleta mambo ya ajabu lakini haitabiriki. Ni vigumu kuitabiri bahati. Twahimizwa tujitahidi bila kutegemea miujiza.

Vinginevyo "Bendera ipepeayo sana mwishowe huchanika." Maana yake bendera au beramu inayopepea sana mwishowe huchanika. Methali hii huweza kutumiwa kumpigia mfano mtu anayejisifu na kujitangaza kwa uwezo alionao. Hatimaye uwezo huo utaisha na abakie katika hali duni au mbaya.

Methali ifuatayo yazihusu Simba na Yanga. "Muungwana ni kitendo." Maana yake muungwana hasemisemi tu bali hulifanya jambo fulani. Methali hii hutumiwa kutushauri tuyafanye mambo tuyasemayo au tusiwe na tabia ya kusemasema badala ya kutenda. Mtu huthaminiwa kutokana na matendo yake bali sio maneno ayasemayo.

**marobarnabas@yaho.com**
**0784 344 096**

HABARI KITAIFA

# Majaliwa aitaka sekta binafsi kuanika vikwazo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imeitaka sekta binafsi kufunguka vikwazo vinavyowakabili ili vitatuliwe na kusaidia kukabiliana na tatizo la ajira nchini.

Aidha, imevitaka vyuo vya elimu ya ufundi kutoa elimu bora inayokidhi viwango na ubora unaotakiwa ili kukidhi mahitaji ya soko la ajira la ndani ya nchi.

Akizindua maonyesho ya pili ya elimu ya ufundi yaliyoandaliwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) kwa kushirikiana na Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF), Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alisema milango ya serikali kushirikiana na sekta binafsi iko wazi na lazima ishirikishwe kwenye mipango ya serikali. "Lengo la serikali chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan ni kuhakikisha sekta binafsi inapewa kipaumbele ili kutoa mafunzo kwa vijana mbalimbali nchini ili wajiajiri badala ya kusubiri kuajiriwa," alisema.

Alisisitiza: "Natoa wito kwa sekta binafsi nchini kama mnakabiliana na changamoto njooni ili mtueleze ili tuangalie namna ya kuzitatua katika kukabiliana na changamoto za ajira."

Alisema sekta binafsi ina mchango mkubwa katika maendeleo ya taifa na serikali imeboresha mazingira ya uwekezaji kwa sekta ya elimu nchini.

Aidha, alisema utoaji elimu ya ufundi unapaswa kutoa majibu ya matatizo ya jamii kwa kuwa tatizo la ajira lipo kwa nchi zote ulimwenguni na ili kukabiliana na tatizo hilo ni kujenga viwanda.

"Wananchi wanaweza kupambana na changamoto za sasa za ajira, elimu wanayopata iwaandae kuwa utengenezaji wa ajira badala ya kutembea kuzitafuta wakati tuna fursa ya kufanya hivyo wenyewe," alisema.

Alisema milango ya uwekezaji wa viwanda ipo wazi na itasaidia kutatua tatizo la ajira kutokana na mikakati inayofanyika ya kukuza ujuzi. Hata hivyo, alitaka NACTE kutumia mamlaka yake kisheria kwa kuzalisha vijana wenye ujuzi stahiki na kubuni mikakati mbalimbali ya kuweka karibu taasisi zote.

"Tumeona ushiriki wa vijana wa kike na kiume wanavyoweza kushiriki kwenye utafiti wa gesi na mafuta, Watanzania hatuna sababu ya kujidharau tunaweza, lazima tutembee tukijua uwezo tunao," alisema.

Naye Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, alisema wizara hiyo itahakikisha kuwa inaendeleza utoaji elimu ya ufundi kwa kuzingatia mahitaji ya soko na kuandaa vijana ili kulipatia taifa rasilimali watu yenye sifa stahiki kwa maendeleo ya nchi. Awali Mwenyekiti wa Baraza la Uongozi NACTE, Prof. John Kondoro, alisema mafunzo ya ufundi yanatolewa katika vyuo 430, huku akisisitiza kuwa NACTE itaendelea kusimamia utoaji wa mafunzo kwa ubora unaotakiwa ili kukidhi mahitaji ya ndani na nje.

Alisema mitaala ya vyuo hivyo itatoa fursa ya wananchi kujifunza kwa vitendo na sio nadharia.

"Tatizo kubwa linalokabili vyuo vya elimu ya ufundi ni ukosefu wa nafasi za mafunzo ya vitendo na inatokana na ushiriki mdogo wa wadau na kukwepa gharama, pia wanafunzi kushindwa kumudu gharama za mafunzo hayo," alisema.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akipata maelezo kutoka kwa Naibu Mkuu wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (Taaluma, Utafiti na Ushauri), Dk. Prosper Mgaya (kushoto), kuhusu ubunifu uliofanywa na chuo hicho wa kutengeneza taa za kizuia magari kwenye makutano ya reli na barabara ili kuepusha ajali, katika maonyesho ya pili ya elimu na mafunzo ya ufundi, kwenye Uwanja wa Jamhuri, jijini Dodoma jana. Watatu kushoto ni Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako. **PICHA: OWM**

# Muhimbili yapunguza vifo vya watoto wa uangalizi maalum

**Na Romana Mallya**

KITENGO cha watoto wanaohitaji uangalizi maalum (PICU) katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, kimepunguza idadi ya vifo vya watoto kutoka asilimia 65 hadi kufikia asilimia 36.4 baada ya kuwahudumia 1,140.

Watoto hao ni wale wanaosumbuliwa na magonjwa mbalimbali wakiwamo wa nimonia, maambukizi kwenye damu na homa ya uti wa mgongo.

Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Tumaini la Maisha, Gerald Mongella, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa maadhimisho ya Siku ya PICU Duniani yaliyofanyika Hospitali ya Muhimbili.

Mongella alisema kitengo hicho ni sehemu ya kuongeza maisha yao ambapo tangu kuanzishwa kwake mwaka 2019, kimehudumia watoto 1,140 na kupunguza idadi ya vifo kutoka asilimia 65 hadi asilimia 36.4.

"Ukitazama idadi ya watoto waliohudumiwa na PICU unajiuliza isingekuwapo ingekuaje. Kipimo cha mafanikio ya kitengo hiki ni kwamba kabla hakijaanzishwa ilikuwa ukipita barabara za ndani za Muhimbili hukosi mama amebeba mtoto anakwenda kuhifadhiwa chumba maalum cha maiti lakini kwa sasa inaweza kupita miezi sita kutoona hili," alisema.

Aliwakumbusha madaktari na wauguzi kuzingatia maadili kwa kufuata miongozo yao ya kazi.

Pia aliwaomba wadau waliodhamini shughuli hiyo wajitokeze kusaidia kitengo hicho ili tatizo la vitanda liweze kutatuliwa.

Daktari Bigwa wa Watoto, kitengo cha Uangalizi Maalum (ICU) hospitalini hapo, Evance Godfrey, alisema kitengo hicho huwapokea watoto wanaopata rufani kutoka hospitali mbalimbali nchini na lengo lao ni kupunguza idadi ya vifo kwa asilimia 20.

Alisema matatizo yaliyopo ni huduma ya ICU kwa watoto hazijasambaa, hawana wataalamu wa kutosha na kuomba waliopo waendelee kupewa mafunzo.

Alisema tangu kuanzishwa kwa kitengo hicho wagonjwa wengi wanaowapokea ni nimonia ni asilimia 17, maambukizi kwenye damu asilimia 16 na homa ya uti wa mgongo asilimia 15.

Mkuu wa Kitengo cha PICU, Dk. Yasser Harbesh, aliwashukuru wafanyakazi wa kitengo hicho na wadau wengine ambao wamekuwa wakijitoa kwa ajili ya kusaidia kuhudumia watoto hao.

Katika maadhimisho hayo wafanyakazi bora ni muuguzi Maimuna Yusuph na Daktari Emmanuel Masawe, ambao wote wamepatiwa zawadi maalum kama motisha ya kazi.

Muuguzi Maimuna alisema amefanya kazi hiyo kwa miaka 20 na moja ya tatizo kubwa kabla ya kuanza kitengo hicho ilikuwa ni kitendo cha kuona mtoto anayehitaji huduma ya mashine ya kupumulia au nyingine na kukosa.

# Kilimo yamulika mambo 7 mwakani

**Na Mwandishi Wetu**

WIZARA ya Kilimo imetaja vipaumbele saba vya kimkakati kwa mwaka wa fedha 2021/22, kubwa ikiwa ni mpango wa kuongeza tija katika kilimo kwa kuweka mkazo kwenye utafiti utakaozingatia ugunduzi wa aina za mbegu bora na mbinu za kilimo.

Waziri wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, alipowasilisha bungeni mwanzoni mwa wiki hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake kwa mwaka ujao wa fedha, alisema watafanya utafiti wa mbegu bora zenye tija kubwa, akitolea mfano utafiti wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI).

Alisema utafiti huo umegundua aina za mbegu za muhogo inayozalisha wastani wa tani 22 hadi 50 kwa hekta kulinganishwa na wastani wa tani nne kwa hekta zinazozalishwa sasa na wakulima wengi nchini.

Alitaja kipaumbele cha pili ni kuongeza tija katika uzalishaji wa mbegu bora, wizara ikipanga kuendeleza mashamba 13 ya mbegu ya ASA kwa kuweka miundombinu ya umwagiliaji kwa kutumia fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Umwagiliaji.

Waziri huo alitaja kipaumbele cha tatu kuwa ni kuimarisha huduma za ugani na kubainisha kuwa idadi ya maofisa ugani katika ngazi ya kata na vijiji ni 6,704 ambapo ni ndogo kulinganishwa na mahitaji ya 20,538.

Kipaumbele cha nne ni kuimarisha kilimo cha umwagiliaji, ikipanga kuongeza eneo la umwagiliaji kwa kuhamasisha wadau kuwekeza katika ujenzi miundombinu, uvunaji wa maji na uchimbaji wa visima kwa ajili ya kilimo cha aina hiyo.

Waziri huyo alisema kipaumbele kingine ni kutafuta masoko ya bidhaa za kilimo zinazozalishwa nchini, zikiwamo ngano, alizeti, maharage ya soya na mazao mengine.

Prof. Mkenda alisema eneo lingine la kipaumbele kuimarisha Kilimo Anga kwa ajili ya kudhibiti visumbufu vya milipuko na vihamavyo kama vile nzige, kweleakwelea na viwavijeshi vamizi ambapo wizara imeongeza bajeti kutoka Sh. milioni 150 mwaka 2020/21 hadi Sh. bilioni tatu mwakani ili kununua ndege moja mpya.

Kipaumbele cha saba ni kuimarisha mifumo ya upatikanaji wa mitaji, wizara ikipanga kufanya tathmini ya mifumo ya upatikanaji wa mitaji kwa wakulima wadogo na wawekezaji wengine kwenye sekta.

Alisema wizara imeunda jopo maalum linalohusisha watendaji wakuu wa taasisi za fedha, ambalo litaongozwa na Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, kwa ajili ya kupitia minyororo ya thamani ya mazao na kushauri namna bora ya upatikanaji wa mitaji kwa ajili ya uendelezaji wa kilimo nchini.

## Tathmini hospitali kongwe, chakavu kuwa endelevu

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), inaendelea kuzifanyia tathmini hospitali kongwe na chakavu 43 ambapo kazi hiyo inatarajiwa kukamilika Machi, 2022.

Naibu Waziri wa Ofisi hiyo, Dk. Festo Dugange, aliyasema hayo jana alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Manyoni Mashariki (CCM), Dk. Pius Chaya.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji lini tathmini ya uchakavu wa miundombinu ya Hospitali ya Manyoni itafanyika.

Alisema hospitali hiyo imejengwa tangu mwaka 1973 na bado inaendelea kutoa huduma lakini inakabiliwa na upungufu mkubwa wa wataalamu.

"Nini kauli ya serikali juu ya upelekaji wataalamu," alihoji.

Akijibu, Dk. Dugange alisema serikali imeshaweka utaratibu wa kufanya tathmini kwa hospitali hizo zilizotambuliwa.

"Kazi imeanza na inaendelea tunatarajia ifikapo mwezi Machi, 2022 tutakuwa tumekamilisha na kufanya maamuzi wapi tutajenga hospitali mpya na wapi tutakarabati hospitali zinazohitaji ukarabati," alisema.

Kuhusu upungufu wa wataalamu, Naibu Waziri huyo alisema serikali imeendelea kuomba na kutoa vibali vya ajira ambapo kwa mwaka huu wa fedha 2020/21, wameomba vibali vya watumishi 12,000.

"Tunaendelea na mchakato wa kuajiri watumishi 2,796 wa kada mbalimbali za afya, tutahakikisha hospitali hiyo inapata mgao wa watumishi," alisema.

Katika swali lake la msingi, mbunge huyo alihoji serikali ina mpango gani wa kuanza ujenzi wa hospitali hiyo kwa kuwa hospitali iliyopo haikidhi mahitaji kutokana na uchakavu na ongezeko la watu.

Dk. Dugange akijibu, alisema serikali inatambua uwepo wa hospitali 43 kongwe na chakavu za halmashauri ikiwamo Manyoni.

"Serikali inaendelea kufanya tathmini ya miundombinu ya hospitali hizo ili kuona namna bora ya kuziboresha ikiwamo kuzikarabati au kujenga hospitali mpya kulingana na matokeo ya tathmini," alisema.

Hata hivyo, alisema serikali imepanga kukamilisha kwanza ujenzi wa hospitali katika halmashauri 28 zisizokuwa na hospitali za halmashauri na kisha hospitali chakavu zitawekewa mpango.

# Taasisi za umma zachangia migogoro ardhi kwa 39%

BUNGE limeelezwa kuwa taasisi za umma ambazo zinadaiwa fidia ya utwaaji ardhi na wananchi zinazochangia asilimia 39 migogoro yote nchini.

Kufuatia hali hiyo, serikali imezitaka kuacha kuchukua ardhi za wananchi bila kulipa fidia na taasisi zinazodaiwa fidia kulipa mara moja vinginevyo maeneo hayo yatarejeshwa kwa wananchi.

Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angelina Mabula, aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Jacqueline Kainja.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji lini serikali itamaliza migogoro ya ardhi katika mikoa ya Tabora na Singida ili wananchi waweze kufanya shughuli zao kwa utulivu na amani.

Akijibu, Mabula alisema serikali inatambua kuwa imekuwapo migogoro ambayo kwa muda mrefu haikuwa imepatiwa ufumbuzi katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara iliagiza ofisi zote za ardhi za mikoa nchini ikiwamo Singida na Tabora kuanzisha jedwali la migogoro ya ardhi ili kuibainisha na kuitatua.

Alisema kwa Mkoa wa Tabora, jumla ya migogoro 211 iliorodheshwa na kati ya hiyo migogoro 102 ilipatiwa ufumbuzi.

Aidha, alisema kwa Mkoa wa Singida jumla ya migogoro 226 imetambuliwa na kati ya hiyo migogoro 34 imetatuliwa na iliyobaki asilimia 85 inatokana na madai ya fidia ambayo wananchi wanadai halmashauri na taasisi mbalimbali za serikali.

Aidha, alisema mkakati wa wizara katika kupunguza au kumaliza kabisa tatizo la migogoro ya ardhi nchini ni pamoja na kuongeza kasi ya upangaji.

Pia alisema upimaji na umilikishaji ardhi kwa wananchi, kuzitaka taasisi za umma kulipa fidia ya wananchi kwa wakati, kuendelea kutoa elimu kwa umma, kushirikiana na serikali za mitaa kudhibiti ujenzi kwenye miundombinu ya umma kama shule, viwanja vya michezo, maeneo ya wazi.

Hata hivyo, alisema wizara za kisekta hushughulikia kero za makundi mbalimbali ya watumiaji ardhi kama wafugaji na wakulima na maeneo ya hifadhi.




**Habari zote na Augusta Njoji,** DODOMA



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki (kushoto), akizungumza na watendaji wakuu wa wizara hiyo, nje ya ukumbi wa Bunge, jijini Dodoma jana, baada ya kupitishwa kwa bajeti ya wizara hiyo ya mwaka 2021/2022. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Singida Mashariki yataka kasi usambazaji umeme

MBUNGE wa Singida Mashariki (CCM), Miraji Mtaturu, amehoji serikali lini itafikisha umeme katika vijiji 28 ambavyo havijapata umeme kati ya vijiji 50 vya jimbo hilo.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato, alisema serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) inaendelea kupeleka umeme vijijini na kuufikisha katika vijiji vyote vya Tanzania Bara ifikapo mwezi Desemba, 2022.

Alisema jimbo hilo lina jumla ya vijiji 50 na 22 tayari vina umeme.

"Vijiji 12 vinapatiwa umeme kupitia Mradi wa Ujazilizi ulioanza kutekelezwa katika Mkoa wa Singida mwezi Novemba, 2020 na unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2021," alisema.

Aidha, alisema vijiji 16 vilivyobakia vinapatiwa umeme kupitia utekelezaji wa mradi wa REA wa kusambaza umeme vijijini awamu ya tatu mzunguko wa Pili ulioanza kutekelezwa mwezi Machi, 2021 na utakaokamilika mwezi Desemba, 2022.

Alisema gharama ya mradi ni Sh. bilioni 8.47.





Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino, mkoani Dodoma, Kenneth Yindi, akitoa taarifa ya utekelezaji wa shughuli zilizotekelezwa na kamati ya kudhibiti Ukimwi katika kikao cha Baraza la Madiwani, wilayani humo juzi.
**PICHA: PETER MKWAVILA**

# Makandarasi wa visima vya maji wapewa sharti kulipwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WIZARA ya Maji imewaagiza Wakala wa Uchimbaji Visima nchini (DDCA) kukusanya hati za madai ya makandarasi wa uchimbaji visima vya maji, ili ifikapo mwezi ujao wawe wameshalipwa madeni yao.

Aidha, amewaagiza DDCA, kuhakikisha wanagawa kazi kwa makandarasi wazawa wenye kukidhi vigezo ili kuhakikisha miradi ya uchimbaji visima inakamilika kwa wakati.

Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akifungua warsha ya wadau wa maji, kuhusu utafiti na uchimbaji wa visima ya maji nchini.

Aweso aliagiza kukusanywa hati hizo haraka ili makandarasi walipwe fedha zao.

Hata hivyo, alisema ni lazima hivi sasa kuwa na teknolojia ya kisasa, mtu anapofanya kazi lazima alipwe kwa wakati ili kazi ifanyike kwa ufasaha.

"Malipo ya kazi yanapaswa kuja kwa wakati hakuna sababu ya kuyachelewesha, ndio maana nawaagiza mkusanye certificate za madai yao kutoka kwa makandarasi ili walipwe na tuanze upya katika kufanya nao kazi ambazo watakuwa wamepewa na wizara."

"Nawaomba ili ninaloagiza lifanyike kwa haraka na muanze kukusanya certificate za hawa waliokuja katika warsha hii ikiwamo kuangalia

namna ya kuwapa kazi wazawa ya uchimbaji visima," alisema Aweso.

Kuhusu DDCA kugawa kazi za uchimbaji visima, Waziri Aweso aliwataka wakala hao kugawa kazi kwa makandarasi binafsi ili kurahisisha upatikanaji wa huduma ya maji mjini na vijijini kwa wakati.

Aweso alisema DDCA inapaswa kuangalia ina uwezo wa kuchimba visima vingapi na vilivyobaki kuwapa makandarasi binafsi wenye nia na uwezo wa kufanya kazi hiyo kwa wakati.

"Katika bajeti ya 2021/2022 mmepewa kuchimba visima 1000 naomba mseme mnavyoweza kuchimba, vinavyosalia wapeni wazawa wenye vigezo na sio kubaki na idadi hiyo ili kutengenezea posho ya siku ya kujikimu," alisema Aweso.

Alisema wanatakiwa kufanya hivyo ili kuepusha kazi hiyo kufanyika kwa muda mrefu na kuchelewesha upatikanaji wa maji katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

"Ninaomba DDCA mkatekeleze hili nililowaambia msiliache hivi ili kutengeneza siku nyingi za kufanya kazi jambo ambalo halikubaliki, kisima mnachimba mwezi mzima ilhali sehemu nyingine mkandarasi binafsi anaweza kuchimba kwa muda mchache," alisema Aweso.

Alisema kuna baadhi ya maeneo kweli unaweza kuchimba visima ndani ya muda huo, lakini maeneo mengine makandarasi huweza kuchimba kwa siku chache tofauti na wao.

Aliwataka DDCA kwenda kufanya utafiti wa usajili wa kampuni za uchimbaji visima, kujua wangapi wamesajiliwa na wangapi hawajasajiliwa, kwa sababu takwimu zilizopo na kuna utitiri wa kampuni za uchimbaji visima.

"Naomba mkafanye utafiti kwa kina kujua kampuni ngapi zimesajiliwa na kufanya kazi, ili tuepushe kazi feki zinazofanywa na makandarasi ambao

hawajasajiliwa na kuleta matatizo ndani ya wizara," alisema Aweso.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Anthony Sanga, alisema makandarasi hao ni sehemu ya wizara hiyo hivyo wasisite kutoa ushirikiano pale wanapoona

kuna kero mbalimbali zinajitokeza.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Rasilimali za Maji, Dk. George Lugomela, alisema watashirikiana na watu hao ili kuhakikisha kazi za uchimbaji visima inafanyika kwa wakati.

# Mkakati waanza kukabili uvamizi wanyama wakali

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

SERIKALI imezindua namba maalumu zitakazosaidia wananchi kuripoti matukio ya kuvamiwa na wanyamapori wakali na majangili kwenye maeneo yao.

Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa.

Dk. Ndumbaro alisema serikali imebuni utaratibu huo wa kuanzisha namba maalumu zitakazowasaidia wananchi kutoa taarifa kwa idara ya maliasili ili kuwaondoa kwenye maeneo hayo waliyovamia.

"Mpango wa Serikali ni kuwadhibiti wanyamapori hawa wakali na waharibifu wa mazao ya wananchi ili kujenga mahusiano mema nao," alisema.

Alibainisha kuwa ili kukabiliana na tatizo la wanyamapori hao ambao wamekuwa wakivamia makazi ya watu na kuharibu mali zao serikali imebuni mpango huo ili kupata taarifa za matukio hayo.

Kadhalika, wananchi watapiga simu bure na zitakuwa kwenye kanda zote za uhifadhi nchini.

Aidha, alisema wizara inaendelea kutoa elimu kwa wananchi kwenye maeneo ya Lindi, Morogoro, Mtwara, Tunduru na baada ya hapo wataendelea na mengine. Aliwaonya wananchi kuhakikisha simu hizo zitatumika kwa makusudi hayo tu, na kwamba watakaojaribu kuchezea watashughulikiwa kwa mujibu wa sheria za matumizi ya mitandao ya simu.

Upande wake, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Allan Kijazi, alisema watendaji wa wizara hiyo wamejipanga na watakuwa wakifika eneo husika kwa wakati. Dk. Kijazi alisema ikitokea kuwa kuna uhitaji wa simu hizo zaidi, Wizara itakuwa tayari kuziongeza ili kupambana na matukio hayo.

# Asasi za mazingira zaonywa kujihusisha na masuala ya siasa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

OFISI ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), imezitaka asasi za kiraia zinazotekeleza miradi ya mazingira kufanya kazi kwa mujibu wa usajili na kuacha kujihusisha na masuala ya siasa.

Mkurugenzi wa Mazingira wa Ofisi hiyo, Dk. Andrew Komba, aliyasema hayo katika kikao baina ya Waziri wa Ofisi hiyo, Selemani Jafo na wawakilishi wa asasi hizo.

Alisema kuwa pamekuwapo na tatizo la baadhi ya asasi hizo zilizosajiliwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya mazingira kufanya shughuli ambazo siyo sehemu ya usajili wake.

"Kumekuwapo na changamoto ya asasi za mazingira ambazo zimesajiliwa kufanya kazi za mazingira lakini unakuta zinafanya vitu vingine kama masuala ya siasa hali ambayo inaondoa tija katika maeneo zilikosajiliwa," alisema.

Alisema asasi za mazingira zinatakiwa kufanya kazi kama ambavyo vibali vyake vya usajili vinavyoelekeza na siyo vinginevyo.

Dk. Komba alisema tatizo jingine ni asasi za mazingira kutekeleza miradi ambayo siyo vipaumbele vya serikali katika maeneo mengi nchini.

Alisema kutokana na hali hiyo, ipo haja kwa asasi za mazingira kuhakikisha zinashirikiana na serikali katika kuibua miradi hiyo ili iwe na tija kwa jamii na taifa kwa ujumla.

"Changamoto nyingine ni kukosekana kwa mawasiliano ya mara kwa mara baina ya Asasi za mazingira pamoja na serikali hivyo kuwa vigumu kutambua mchango ulifanywa na Asasi katika sekta ya mazingira," alisema.

Vile vile, alisema kumekuwapo na tatizo kwa asasi hizo kupeleka miradi katika maeneo ambayo hayana uhitaji, hivyo kukosekana kwa ufanisi wa miradi.

Alisema kuwa ili kuondokana na tatizo hilo, ipo haja kwa serikali kushirikishwa katika miradi hiyo ili kuweza kushauri na kupeleka miradi katika maeneo yenye uhitaji na kuoka fedha ambazo zingetumika vibaya.

Awali, akifungua kikao hicho, Waziri Jafo, alisema lengo ni kufahamiana kati ya Ofisi ya Makamu wa Rais pamoja na wawakilishi wa asasi za kiraia zinazotekeleza miradi ya mazingira nchini.



# Uhaba wa wataalamu waathiri sekta kilimo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Dk. Soud Hassan Nahoda, amesema kuna upungufu wa wataalamu bingwa wenye Shahada ya Uzamivu (PhD) na kusababisha wakulima kukosa mbinu za kisasa za kilimo chenye tija.

Dk. Nahoda alisema hayo wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Ziwani, Suleiman Makame, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, ambaye alisema wakulima wengi katika kisiwa cha Pemba hawajafikiwa na huduma za wafanyakazi wa sekta ya kilimo.

Waziri huyo alisema mpaka sasa wana wataalamu bingwa watano wenye Shahada ya Uzamivu wanaotoa huduma katika wizara na hiyo inatokana na wafanyakazi kustaafu kwa mujibu wa sheria za utumishi.

Pia alisema ufinyu wa nafasi zinazotolewa na serikali kwa wanafunzi wa elimu ya juu ndani na nje ya nchi nayo zimechangia kukosekana kwa wataalamu wenye kiwango hicho cha elimu.

"Tatizo hili lipo pia kwa wasomi wa shahada ya pili ambao wengi wao wameanza kustaafu na wengine kukimbia nchi kwenda kufanya kazi katika nchi jirani za Afrika ya Mashariki na Ulaya," alisema.

Waziri huyo aliiomba serikali kusomesha vijana wengi katika fani ya kilimo na mifugo ya viumbe mbalimbali kwa lengo la kujitosheleza katika maeneo hayo ili wananchi wanufaike na utaalamu wao.



Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Muhammed Said, akijibu swali aliloulizwa katika kikao cha Baraza la Wawakilishi Chukwani Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Hemed kukabidhiwa muswada Sheria ya Habari

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Habari, pamoja na mambo mengine atakabidhiwa muswada wa Sheria mpya ya Habari Zanzibar.

Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya maadhimisho hayo, Dk. Mzuri Issa, alisema sherehe hizo zitafanyika Jumapili na kutakuwa na tunzo za umahiri wa waandishi wa habari Zanzibar.

Suleiman alisema muswada huo ambao umebeba miongozo na maazimio ya habari kikanda, kimataifa pamoja na mazingira ya Zanzibar, umekamilika na unategemewa kukabidhiwa rasmi kwa kiongozi huyo.

Alisema muswada huo ukipitishwa kuwa sheria utaweza kufuta sheria namba tano ya magazeti ya mwaka 1988 na vifungu vya sheria ambavyo vimepitwa na wakati na havitoi mazingira mazuri kwa sekta ya habari kufanya vizuri.

"Waandishi wa habari ni kada muhimu katika kukuza na kuendeleza maendeleo ya nchi ikiwamo kidemokrasia, uwazi, uwajibikaji na shughuli za kiuchumi, hivyo waandishi hawana budi kutekeleza majukumu yao chini ua mfumo mzuri wa sheria ambao utawalinda," alisema.

Dk. Mzuri alisema suala la kuwa na sheria ya habari mpya, limekuwa katika mchakato na kupitia hatua mbalimbali zilizochukuliwa zilizohusisha ukusanyaji wa maoni ya wadau.

Kuhusu tunzo za umahiri wa uandishi wa habari, alisema kuwa majaji wameshamaliza kazi yao na kazi 52 zimewasilishwa ambapo washindi watangazwa kesho katika maadhimisho ya uhuru wa habari.

Alisema tunzo hizo zinashindaniwa katika makundi matano ikiwamo uchumi wa buluu, serikali ya umoja wa kitaifa, jinsia, rushwa na tunzo ya kodi.

Maadhimisho hayo yameandaliwa na Jumuiya ya Waandishi wa Habari za Maendeleo Zanzibar (WAHAMAZA), Klabu ya waandishi wa habari Zanzibar (ZPC), Klabu ya Waandishi wa Habari Pemba (PPC), Idara ya Mawasiliano na Mafunzo ya Habari Zanzibar, Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA, Zanzibar) na Baraza la Habari Tanzania Ofisi ya Zanzibar.

# SMZ yafunguka nafuu maambukizi ya corona

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya, Jinsia, Wazee na Watoto, Nassor Ahmed Mazrui, amesema katika kipindi cha mwezi huu hawajapata mgonjwa yeyote wa corona, na kuwataka wananchi kuendelea kuchukua tahadhari ya kujikinga.

Mazrui alitoa maelezo hayo jana wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo Kwahani, Rashid Abdallah, aliyetaka kujua kwa nini wananchi wanaokwenda nje wanatozwa Sh. 180,000 kwa ajili ya kipimo cha corona na kuitaka serikali kutoa msimamo wa chanjo kwa mahujaji watarajiwa.

Akijibu swali hilo, Waziri Mazrui alisema pamoja na kwamba mwezi huu wa Mei Zanzibar haijapata mgonjwa wa corona, nchi nyingine duniani bado ipo na kutaka tahadhari zinazotolewa na wataalamu wa afya ziendelee kufuatwa.

Aliwakumbusha wananchi kuendelea kuvaa barakoa, kunawa mikono mara kwa mara kwa maji tiririka na kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima ili kujikinga na ugonjwa huo.

Kuhusu chanjo ya corona, Waziri huyo alisema serikali imeridhia wananchi wake kuchanjwa chanjo hiyo na kwamba hivi karibu wataalamu wa afya na mahujaji wanaotarajia kwenda Maka kuhiji wataanza kuchanjwa. Pia alitaja kundi lingine litakalofuata kupata chanjo hiyo ni watoa huduma wa sekta ya utalii, wazee kuanzia miaka 50 na wananchi. "Chanjo ya corona ni muhimu, serikali itahakikisha chanjo itakayotolewa haina madhara na tayari, Shirika la Afya Duniani (WHO) limeshathibitisha kampuni nne ambazo zinatoa chanjo na hazina madhara yoyote," alisema. Alisema Serikali ya Zanzibar imeondoa gharama ya kipimo cha corona kwa wanafunzi wanaosoma nje ya nchi pamoja na wagonjwa wanaokwenda huko kwa matibabu ambao wanatambuliwa serikalini.

Waziri Mazrui alisema kumejitokeza baadhi ya watu wasiyo waaminifu hutoa vyeti bandia vya majibu ya upimaji wa corona na hadi sasa wamevikamata zaidi ya 200. Alisema vyeti hivyo vimekuwa vikitumika kuwapa wasafiri na tayari kituo ambacho kimekuwa kikifanya hivyo wameshakidhibiti.

Akichangia bajeti ya wizara hiyo, Mwakilishi wa Jimbo la Chaani, Nadir Abdul-Latif, alisema hayupo tayari kuchanjwa chanjo ya corona kwa sababu nchi mbalimbali duniani wananchi wake waliopatiwa chanjo hizo zimewaletea madhara na wengine kufa.

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE



GRAY WA 'EMPIRE' MATATANI TENA Uk.14






YAMEISHAA!

# Chege, Nature waligombea mrembo miaka 10

KIONGOZI wa kundi la TMK Wanaume Family na Meneja wa Diamond Platnumz, Mkubwa Fella, amesema tofauti zilizokuwapo kwa muda wa miaka kumi kwa wasanii wake Chege na Juma Nature sasa zimekwisha.

Wasanii hao kwa kipindi chote wamekuwa maadui kutokana na kile kinachoelezwa kuwa ni kugombea mwanamke.

Akizungumza na Nipashe jana, Fella amesema wasanii hao walikuwa wakikutana na kusalimiana, lakini ukaribu wa kufanya nyimbo au kukaa pamoja haukuwapo.

"Hakuna hata cha kuficha bana, hawa tatizo lao lilianzia kwa mwanamke, Chege alikuwa na mwanamke wake ambaye baadaye alikuja kumpenda Juma Nature ambaye kipindi hicho alikuwa staa kuliko wenzake kundini, baadaye Nature akajikuta ameoa kabisa huyo binti (bila kumtaja jina)," amesema Meneja huyo ambaye ni diwani kata ya Kilungule.

Amesema mwaka huu, Chege alifiwa na mama yake na Juma aliweza kushiriki maziko hayo pasipo kuonyesha tofauti.

"Mwaka huu ndio wamekutana na kwenye msiba wa Mama yake Chege na kuamua kuweka tofauti zao pembeni na kufanya kazi mpya iitwayo 'Kucha", ameongeza.

Hata hivyo, ameeleza tofauti zao ni jambo la kawaida kwa kila binadamu.

"Tofauti za kawaida sana, sema waja wamezikazia sana, na siye kwa vile kioo cha jamii tumebaki kukaa kimya na maisha yanaendelea, na ili kuthibitisha kwamba siye ndugu tayari tumewaletea song jipya linaitwa Kucha litakalozungumzia mapenzi," amesema Chege ambaye jina lake halisi ni Said Juma.

BASI SAWA

## Mshana kuja na Qaswida



MSANII chipukizi wa muziki wa Qaswida, Badi Mshana, Maarufu kama 'Mshanatz, anajiandaa kutambulisha wimbo wake mpya unaoitwa 'Nafsi' ambao upo katika hatua ya mwisho.

Akizungumza na BT, Mshana amesema wimbo huo unazungumzia namna familia nyingi zilivyojisahau na kuacha misingi inayompendeza Mungu kimaadili.

"Familia yangu imeegemea sana katika dini, isitoshe nimesoma katika mazingira hayo imekuwa rahisi kuimba nyimbo za Qaswida ambazo zinalenga kumjua Mungu," amesema Mshana.

Wimbo huo umerekodiwa na studio ya Badru Studio ya Kigogo na video imeandaliwa chini ya mwongozaji YHD wa jijini Dar es Salaam.

## Machozi na Kuchi kichwani



MWANAMUZIKI mkongwe, Hussein Machozi, ambaye hivi karibuni ametambulisha mtindo wake mpya wa nywele na kuutaja sawa na kuku kuchi.

"Nimeamua kuweka mtindo huu wa nywele niliouita kuchi, neno hilo ni nyoya la kuku ambaye akipigana huwa anahakikisha anashinda hata kama akifa, lakini kikubwa ashinde, na mimi nimeliweka hili nyoya nikimaanisha sichoki mpaka nishinde," amesema Hussein Machozi.

Msanii huyo ambaye aliweka makazi yake nchini Italia, ameingia nchini hivi karibuni lakini hajaelezea kama atarudi katika ulingo wa muziki.

Ameongeza kuwa wakati anaishi nchini humo alikuwa anafanya kazi ya kufundisha watu kuteleza kwenye barafu.



# Chege, Juma Nature watabiri ujio mpya

WAKONGWE wa muziki wa kizazi kipya, Juma Nature na Chegge Chigunda, wamewataka mashabiki kuangalia mbele na kuacha kuhoji kwa nini wako pamoja tena.

Wasanii hao wamesema hayo baada ya kutambulisha wimbo unaitwa 'Kucha', ambapo wameeleza kuna mambo makubwa yanakuja, hivyo watu wasubiri kwa hamu.

"Mtu kuhoji kwa nini tulisambaratika ni sawa na kupoteza muda, ila jambo la msingi ni kuangalia ya mbele hasa wakati huu ambao tumeamua kuja upya tukiwa na wimbo wa Kucha," amesema Nature.

Upande wa Chegge, amesema wanajiandaa kushirikisha wasanii wachanga kwenye baadhi ya nyimbo wanazoziandaa ili kupata vionjo tofauti na kuwasaidia kupata umaarufu kwenye muziki huo.





## Kaniki Nyeusi; Ukificha dawa, ukivaa majanga

**Na Adam Fungamwango**

KILA sehemu ina utaratibu wake. Ndiyo maana katika dunia hii kila nchi utakayokwenda unakutana na sheria tofauti. Kuna nchi kumuadhibu mtoto wako ni jambo la kawaida tu kama hapa kwetu kama ni kwa kumjenga si kwa kumdhuru. Hata hivyo kuna nchi ukimpiga mtoto wako kwa sababu yoyote ile ni kosa na unaweza kufunguliwa mashtaka.

Filamu yetu ya leo tutakayoiangalia ni 'Kaniki Nyeusi'. Baadhi ya wasanii walioicheza ni Faraja Msongela, Grenda Mushi, German Adam, Juma Said na wengineo.

Kwenye kijiji kimoja cha Manoelo ambacho mwenyewe aliyekivumbua au mwanzilishi wa kijiji hicho alitaka kila anayeishi hapo avae nguo aina ya kaniki.

Alikuwa na sababu kwani, kuna mzimu ambao huwadhuru wote ambao wanakiuka sharti la kutovaa kaniki.

Hata kizazi kilichofuatia waliendelea kutekeleza mila hiyo. Haikukatazwa mwanakijiji akitoka ndani ya kijiji hicho asivae, ila anapokuwa ndani ni lazima avae. Si mwanaume, mwanamke, kijana au mzee.

Kuna mlevi mmoja anaitwa Kagame, yeye alikuwa hataki kabisa kuvaa mavazi hayo. Akavaa anavyojua mwenyewe. Kilichompata, mwenyewe alikubali.


Kuna mama mmoja ambaye alikuwa na binti yake aitwaye Nyendo. Yeye alipata bahati na kwenda mjini.

Baada ya miaka mingi alirejea akiwa na mchumba wake Fred. Pamoja na kwamba alikaribishwa vizuri, lakini alikumbushwa kuwa baada ya siku moja tu, adumishe mila kwa kuvaa kaniki ili waweze kuwa salama.

Walikataa na kuendelea kuvaa mavazi yao ya mjini. Mama Nyendo aliitwa na Mwenyekiti wa Kijiji na kuambia amwonye binti yake, lakini binti na mpenzi wake alikataa. Waliendelea kuaa viwalo vya kisasa.

Siku isiyo na jina walikuwa na matembazi yao ya kawaida, Fred alianguka na kuzirai. Hali hiyo ilileta taharuki na kupelekwa na mganga ambaye aliwaambia kuwa lazima mila zidumishwe, mgeni huyo na Nyendo wavae kaniki.





# Dogo Janja apagawa mauzo ya albam

KATIKA jambo linalomfurahisha Dogo Janja ni kuona album yake ya 'Asante Mama', inazidi kufanya vizuri katika mauzo.

Album hiyo yenye nyimbo 11, mpaka sasa imeuzwa nakala zaidi ya laki moja kwenye mtandao wa kupakua muziki wa Boomplay.

Dogo Janja amekuwa tofauti kwa kuwashirikisha wasanii wakubwa wa kike nchini kama Mimi Mars, Nandy, Maua Sama, Khadija Kopa, Lulu Diva, Rosa Ree, Lady Jaydee na Linah.

# Midomo ya bata pambe

**Na Adam Fungamwango**

HATA kwenye muziki wa dansi kwa sasa chombo cha saxophone hakitumiki sana. Labda unaweza kukiona kwenye bendi kongwe kama Msondo Ngoma Music Band na DDC Mlimani Park Orchestra.

Lakini ni chombo kilichotumika karibuni na bendi zote za dansi za zamani. Kama bendi haikuwa na trumpet na saxophone, basi haikuhesabika kama bendi iliyokamilika.

Mashabiki walikipenda sana chombo cha saxophone na wapigaji wake. Chombo chenyewe kikabatizwa jina kikaitwa 'mdomo wa bata'. Mwanamuziki anayekuwa anapuliza chombo hicho akaambiwa 'anatafuna muwa'.

Siku za hivi karibuni tuliona hata wanamuziki kama Diamond, Ommy Dimpoz na wengineo walitumia chombo hicho kwenye baadhi ya nyimbo zao.

Wapo wanamuziki wengi nchini Tanzania walikuwa na uwezo mkubwa na kupiga au kupuliza chombo hicho, lakini leo tutaangalia wale ambao wanaaminika kuwa walikuwa juu zaidi ya wenzao.

**TWAHIR MOHAMED**

Anasadikiwa kuwa ndiye mpuliza midomo ya bata namba moja nchini Tanzania. Na inawezekana ikawa Afrika Mashariki. Inasadikiwa hadi sasa hawajawahi kupatikana mpigaji kama yeye. Twahir ambaye mwongo mmoja kuanzia mwaka 1980 hadi 1990 alipiga zaidi kwenye bendi cha Orchestra Safari Sound kwenye awali wa 'Masantula' iliyokuwa ikiongozwa na Kikumbi Mwanza Mpango 'King Kiki' na 'Dukuduku' iliyokuwa ikiongozwa na Freddie Ndala Kasheba. Mbali na uwezo mkubwa, lakini alikuwa na pumzi ya kupiga chombo hicho mwanzo wa muziki hadi mwisho. Ushahidi sikiliza wimbo wa 'Mimi Msafiri'. Alifia na kuzikwa nchini Kenya, ambako alikwenda kupigia bendi mbalimbali, ikiwamo Simba Wanyika.

**ABDALLAH KIMEZA**

Ni mmoja kati ya wapiga sax maarufu miaka ya 1980 hadi mwishoni mwa miaka hiyo. Ana heshima kubwa nchini Tanzania. Kimeza ambaye ameshafariki dunia, alipigia bendi kubwa za Vijana Jazz, Maquiz du Zaire, na Orchestra Safari Sound. Ukitaka kumsikia kwenye Maquiz, basi sikiliza nyimbo kama 'Kiongo' na OSS sikiliza 'Christina Moshi' ambazo ni moja kati ya nyimbo alizopiga na anapoanza, waimbaji huwita 'Kimeza njooo…"

**LUZA ELIAS**

Alianzia Jamhuri Jazz. Hakupata jina kubwa sana. Lakini alipokwenda Kenya na kujiunga na Simba Wanyika chini ya Wilson Peter na George Peter 'Kinyonga'. Nyimbo nyingi humtaja na kumuimba 'Luuuza eeee'. Hiyo ilimfanya kujipatia umaarufu mkubwa miaka ya 1970. Miaka ya 1980, aliliacha kundi hilo na kurejea nchini akajiunga na Mwenge Jazz. Ilibidi Simba Wanyika wamchukue Twahir kwenda Kenya kuchukua nafasi yake.

**KHATIB ITEITEI**

Huyu ni mwanamuziki mkongwe kwenye tasnia hii ya muziki, akipiga sax kwenye bendi mbalimbali nchini. Hata hivyo bendi iliyompatia umaarufu mkubwa ni Kyauri Voice ambapo ukizisikiliza nyimbo zote kama 'Mwaka wa Watoto', 'Bangungi', na nyinginezo, Sax imepigwa na mkongwe huyo.

**KING MALUU 'AKULYAKISALE'**

Sina haja ya kumwelezea sana mpiga sax huyu kwa sababu mbali na kupiga bendi kama Maquiz na nyingine nyingi, lakini ndiye aliyepiga sax kwenye ngoma nyingi za bongo fleva za kina Diamond , 'Tupogo' ya Ommy Dimpoz na wanamuziki wengi wa kizazi kipya.





# Ben, Lopez mapenzi njenje

INAONEKANA wazi nyota wa Hollywood Ben Affleck na Jennifer Lopez, wameshibana kimahaba baada ya kuonekana hivi karibuni mjini Miami, wakifurahia maisha.

Kulingana na TMZ, Affleck, aliruka na ndege hadi Miami, siku ya Jumapili iliyopita kwa ajili ya kukutana na J lo, na baadaye nyota hao walionekana katika jumba la kifahari katika ukingo wa maji.

Penzi hilo jipya kati ya Affleck na Jennifer, limeibua mjadala mkali huku wawili hao wameonekana kutoficha hisia zao na kuacha kila kitu wazi.



## Gray wa 'Empire' matatani tena

MWIGIZAJI wa tamthilia ya 'Empire, Bryshere Gray, uhenda akapandishwa kizimbani baada ya kufunguliwa faili la uchunguzi kwa kosa la shambulio.

Grey endapo atakiri kufanya kosa hilo, atatumikia kifungo cha siku 10 jela na kuwekwa katika uangalizi kwa muda wa miaka mitatu.

Awali staa huyo wa filamu wa Marekani, alikuwa katika uangalizi maalum kwa ajili ya kuacha matumizi ya dawa za kulevya, lakini alikamatwa hivi karibuni baada ya kufanya vurugu.

## Mwigizaji mkongwe Nigeria aaga dunia

MWIGIZAJI mkongwe kutoka Nollywood, Ify Onwuemene, amefariki dunia baada ya kuugua saratani kwa muda mrefu.

Taarifa ya kifo chake imetolewa katika ukurasa wa Facebook wa msanii mwenzake, Gloria Anozie Young, ambaye aliandika kuondokewa na shujaa huyo wa filamu.

"Kwa masikitiko makubwa tumempoteza Iffey Onwuemene, ambaye amekwenda katika ufalme wa Mungu," ameandika Gloria.









## Rapa Safaree, Erica watimuana rasmi

RAPA mkali wa Marekani, Safaree na mke wake Erica Mena, wamefungua faili la madai ya talaka mahakamani.

Kulingana na mtandao wa TMZ, Mena ndiye aliyefungua madai hao siku ya Jumanne katika mahakama ya juu ya Fayette County, jimbo la Georgia nchini Marekani, akitaka talaka yake kutokana na kushindwa kuhimili matendo yake.

Mena na Safaree wana mtoto mmoja wa kike mwenye umri wa mwaka mmoja, hata hivyo ndani ya madai hayo anataka kupewa matunzo ya mtoto pamoja na mgawanyo wa mali.

## D Black msimamo huo utawakosa warembo

MSHINDI wa tuzo ya Multiple raia wa Ghana, D-Black, amesema wanawake wenye madoido hawezi kuoa kwa sababu kamwe anaamini wapo kwa kila mwanaume.

Mwana hip-hop huyo ambaye ni CEO wa lebo ya Black Avenue Muzik record. Wanawake wa aina hiyo wanapenda kuvaa viatu virefu na mawigi ya kila rangi, lakini hawana upendo wa dhati.

"Kwa maoni yangu wanawake wajanja wanamtafuta kila mtu kujihifadhi, siwezi kuoa mke wa aina hiyo," ameandika.



**MAKALA**

# Queen Sendiga alipokabiliana vikali mfumo kandamizi kwa wanawake kupata uongozi

**Mary Geofrey**

WANAWAKE wamekuwa wakikabiliwa na changamoto mbalimbali katika kufikia malengo yao, hasa pale wanapotafuta haki zao za uwakilishi katika nafasi za uongozi.

Sehemu kubwa ya jamii yetu nchini, imekuwa ikimwangalia mwanamke katika dhana tofauti na kumhusisha au kudiriki kumtolea hukumu huku akionekana kama kiumbe kisichoweza kuleta maendeleo katika jamii yake.

Miaka ya hivi karibuni tumeshuhudia namna wanawake kadhaa ambao walipata fursa ya kuongoza kwa ustadi na weledi mkubwa pamoja na kukabiliwa na changamoto kadhaa ikiwamo mfume dume.

WataalamU wa siasa nchini wanasema dhana ya kuwa mwanamke hawezi kuongoza, inaweza kuwa historia sasa baada ya Taifa letu kuongozwa na Rais mwanamke, Samia Suluhu Hassan, ambaye hapo awali alikuwa Makamu wa Rais kabla ya kufariki mtangulizi wake, Hayati Rais John Magufuli.

Queen Sendiga ni miongoni mwa wanawake walioingia kwenye historia ya Taifa letu, baada ya kujitosa kuwania nafasi ya urais kupitia Chama cha Alliance For Democratic Change (ADC), katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

Sendiga ambaye alishiriki hadi hatua ya mwisho ya kuwania nafasi hiyo ya juu nchini, anasema licha ya kuwapo kwa changamoto mbalimbali katika kuwania nafasi za uongozi, lakini siyo kigezo cha wanawake kusita kuwania nafasi yoyote.

Anasema changamoto kubwa kama za kuombwa rushwa ya ngono, kutukanwa na kushindwa kufikia malengo zinasababishwa na wanawake wenyewe kushindwa kujiandaa vya kutosha.

Sendiga anaeleza wanawake wanaotaka kuwania nafasi zozote za uongozi wanapaswa kuwa na uelewa mpana wa mambo yahusuyo uongozi.

"Kwa wanasiasa wanapaswa kufahamu vyema katiba, kanuni na mwongozo wa vyama vyao na wao wajiamini na kujitambua katika nafasi wanayotoka kuwania," anasema Sendiga.

Anaeleza kuwa, wanawake ambao wanawania nafasi na hawana uelewa mpana wa mambo ya siasa na wasiyojua ratiba za vyama vyao, ni rahisi kurubuniwa kwa kuombwa rushwa.

"Lakini kwa mwanamke anayejitambua na kufahamu anachokisimamia, anachokitaka na akafahamu vyema katiba na misingi ya chama chake ni ngumu kushawishika kwa rushwa yoyote," anasisitiza Sendiga.

Anasema wagombea ambao ni wanaume wanaangalia madhaifu ya wanawake kabla ya kumwingia kwa ajili ya kumshawishi kumwomba rushwa au kumpa maneno makali ili kumkatisha lengo lake.

Sendiga ambaye kwa sasa ni Mkuu wa Mkoa wa Iringa, anajitapa kuwa kwa sababu alijitambua na kujipanga kabla ya kuwania nafasi hiyo ya juu, hakuna changamoto aliyokutana nayo.

"Nilijipanga vyema kwa hiyo hakuna changamoto iliyonikwamisha kama kuombwa rushwa ya ngono zaidi ya uhaba wa rasilimali fedha," Sendiga anasema.

Anafafanua zaidi kuwa, licha ya kukabiliwa na changamoto ya rasilimali fedha, lakini alifanikiwa kufika maeneo mengi nchini hasa vijijini.

Anasema pia kwa sababu alikuwa akijiamini kwa vile alikuwa anakijua vyema chama chake, alijijengea mvuto wa kipekee kwa jamii.

"Asikuambie mtu mwanamke ukiwa unajiamini, unafahamu kile unataka unakuwa mzuri na mwenye mvuto wa kipekee sana," anasema Sendiga siku chache kabla ya kuteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Iringa.

Anatoa wito kwa asasi za kiraia ambazo zina mchango mkubwa wa kuhamasisha wanawake kuwania nafasi za uongozi, kuwasimamia wanawake wanaojitosa kuwania nafasi za juu za uongozi bila kujali Itikadi za vyama vyao.

"Kama asasi za kiraia zina mchango mkubwa kiasi cha kushawishi wanawake kuwania nafasi za uongozi, makazini na kwenye siasa, Basi waone kuwa Wana jukumu pia la kuhakikisha mwanamke anafikia malengo yake kwa kumshika mkono anapowania," anasema Sendika.

Sendiga ambaye ameteuliwa na Rais Samia kuwa Mkuu wa Mkoa wa Iringa, anasisitiza kuwa, elimu inayotolewa na asasi za kiraia zilenge kuyafikia makundi mengi ya wanawake wenye nia ya kuwania uongozi, lakini wanakosa msukumu.

"Nimekuwa nikishuhudia sana asasi za kiraia zikitoa mafunzo mbalimbali kwa wanawake ili kujitokeza kuwania nafasi za uongozi, lakini changamoto ninayoiona wanafikia makundi yale yale badala ya kutafuta makundi makubwa," anasema Sendiga.

Aidha, anakipongeza Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA) kwa kuwa sehemu ya kusaidia wanawake kujitambua, kuona wanaweza na kustahili kushika nafasi za juu za uongozi.



Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Queen Sendiga.

**TAMWA INAVYOSAIDIA HARAKATI**

Oktoba Mosi, mwaka huu, TAMWA kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa linalohudumia wanawake (UN WOMEN), walizindua mradi wa Uongozi na Ushiriki wa Wanawake katika Siasa.

Mradi huo unahusisha uandaaji wa midahalo ya habari ili kuongeza uelewa wa jamii kuhusu umuhimu wa ushiriki wa mwanamke katika siasa na uongozi pamoja na madhara ya magonjwa ya milipuko kama COVID 19.

Mkurugenzi Mtendaji wa TAMWA, Dk. Rose Reuben, anasema kwa mujibu wa ripoti ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) ya mwaka 2016, inaonyesha kuwa asilimia 17 ya mawaziri ni wanawake, makatibu wakuu ni asilimia 11, wakuu wa mikoa ni asilimia 23, huku wakuu wa wilaya wakiwa ni asilimia 28.

"Hali hii inadhihirisha namna nafasi ya mwanamke ilivyokuwa ndogo, licha ya hamasa zinazoendelea kufanywa na Serikali kwa kushirikiana na Asasi za Kiraia," ansema Dk. Reuben.

Kwa mujibu wa TAMWA, licha ya serikali kuunda sheria zinazowaruhusu wanawake kushiriki nafasi hizo, bado kumekuwa na mwamko mdogo wa ushiriki wao kutokana na mifumo kandamizi iliyopo kwenye jamii dhidi yao.

Mifumo hiyo inakinzana na azma ya kujenga jamii isiyokuwa na ubaguzi kama ilivyobainishwa kwenye dira ya taifa mwaka 2025, Katiba ya nchi ya mwaka 1977 na sheria mbalimbali.

Wakili wa Kujitegemea, Peter Madeleka, anasema sheria za vyama vya siasa hazimnyimi mwanamke kuwania nafasi ya uongozi.

Anasema tatizo analiona kwenye mfumo wa wa kumpata kiongozi ambao wanachama wenyewe wanaamini mwanaume ndiye anafaa kuongoza kuliko mwanamke.

"Sheria za msajili wa vyama vya siasa, Katiba ya nchi na sheria za vyama vya siasa, hazimbagui mgombea yoyote kwa jinsia yake wala kabila lake hivyo tatizo lipo kwenye dhana iliyojengeka kwa jamii yetu," anasema Madereka.



Queen Sendiga akiwa katika kampeni ya kuwania nafasi ya urais katika Uchaguzi Mkuu, 2020.

Anasema ni wajibu wa Taifa zima kuanza Sasa kuweka imani kwa wanawake ambao wanaongozwa na Rais Samia Hassan kuwa wanaweza tena bila kuwezeshwa.

**UN-WOMEN**

Kwa mujibu wa takwimu mpya zilizotolewa na UN -Women hivi karibuni mchakato wa kufikia usawa wa kijinsia katika maisha ya umma na katika ufanyaji maamuzi umekuwa ukijikokota.

Takwimu zinaeleza kuwa hadi sasa duniani kote wabunge wanawake ni asilimia 25 pekee, na nchi tatu tu ndizo zimefikisha asilimia 50. Wanawake wabunge walio chini ya umri wa miaka 30 ni chini ya asilimia moja.

Kwa upande wa wanawake wafanya mazungumzo katika mizozo ni asilimia 13, asilimia sita ya wapatanishi na asilimia sita watia saini katika michakato rasmi ya amani.

Takwimu hizo zinaeleza zaidi kuwa mwaka 2020, asilimia 7.4 tu ya kampuni tajiri 500, duniani ndio zilikuwa zinaendeshwa na wanawake, na ni nchi 22 tu duniani ndizo zinaongozwa na mwanamke.

Aidha, takwimu zinaonyesha Watanzania wote kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012, wanawake ni zaidi ya asilimia 51.

Hata hivyo, katika idadi hiyo ni asilimia 30 ya wanawake wanaoshiriki katika uongozi kwenye vyama vya siasa, Serikali, Bunge, Mahakama na katika nafasi nyingine za uongozi.

Pamoja na dhamira ya Serikali ya kufikia usawa wa kijinsia katika uongozi, yaani 50 kwa 50, hali halisi inaonyesha bado wanawake wako nyuma katika kupigania nafasi za uongozi.

Kubwa zaidi ni azimio la Jumuiya ya Maendeleo ya nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), linalotaka ushiriki wa wanawake na wanaume katika fursa za uongozi kuwa 50 kwa 50 ifikapo mwaka 2030. Hata hivyo bado ushiriki wa wanawake uko chini.

Kwa mujibu wa Ripoti ya Shirika la Kazi Duniani (ILO), imeonyesha kuwa, kampuni za kibiashara zenye uongozi wa ngazi ya juu mchanganyiko wa wanawake na wanaume zinapata faida kubwa.

Ripoti hiyo iliyotolewa Geneva Uswisi, yenye jina "Wanawake katika biashara na Usimamizi, Biashara kwa ajili ya mabadiliko", inatokana na utafiti wa takribani kampuni 13,000 katika nchi 70 Duniani kote.

Zaidi ya asilimia 57 ya washiriki wa utafiti huu walikubali kuwa uwepo wa jinsia tofauti uliboresha matokeo ya biashara ambapo takribani robo tatu ya kampuni zenye mchanganyiko wa viongozi ziliripoti ongezeko la faida kati ya asilimia 5 hadi 20.

# IGP SIRRO ATOA DARASA...

## •Namna jukumu lao kuu Polisi kukabili jinai, yatetea afya yako

**Na Yasmine Protace**

KUNA hatua Jeshi la Polisi inashiriki kuilinda afya ya umma, tena kwa nafasi kubwa. Kwa vipi? Hapo ndipo Inspekta Jenerali wa Polisi (IGP) Simon Sirro ana uchambuzi wake kwamba inaanza na utoaji elimu kwa umma.

Katika hilo, Sirro anasema kuna matunda yanayoshuhudiwa, kwamba ajali hadi sasa zimepungua kwa wastani wa asilimia 35, mbinu mojawapo inayotumika ni kuwatoza faini wasababishaji ajali, hata kufikiwa matokeo hayo ya mafanikio tajwa.

IGP Sirro katika maoni yake kuhusu masuala ya usalama barabarani na jinsi wanavyofanya kazi, ili kuhakikisha ajali haziongezeki.

Anasema, katika usalama barabarani huwa kunakuwapo ajali zinazosababishwa na dereva mwenyewe, pia zinazotokea kutokana na miundombinu iliyopo.

Mkuu huyo wa Polisi anasema, ajali ambayo anatafsiri zinazisababishwa na dereva, ni pale panaonekana makusudi yake na baadhi wanaposimamishwa hudiriki kukimbia.

Ni hatua inayomfanya askari kuchukua usafiri kumkimbiza na Sirro anatolea ufafanuzi kwamba, katika kukimbizana huko inapotokea ajali, basi tafisiri ya chanzo cha ajali kisheria inamuangukia anayekimbia.

"Kama umesimamishwa na polisi unapokimbiza gari, hapo unatengeneza makosa, kwa kuwa ukisimama unakaguliwa na kama hakuna shida utaendelea na safari," anaeleza.

Kwa mujibu wa IGP Sirro, maeneo makuu ambayo huagukia kuwa chanzo cha ajali, ni wanapokabiliwa na sehemu kubwa ya mawazo, hali kadhalika ulevi.



IGP Simon Sirro; ana mengi kuhusu afya ya umma kupitia ofisi yake.

Anasema vyanzo vya ajali nyinginezo, ni madereva wanapokosa sifa za kuendesha gari, lakini mmiliki anamsababishia ajali. Inapofuiatiliwa, huanguka kashfa ya kukosa leseni.

Bodaboda, chombo cha moto kilichotapakaa kila kona nchini hivi sasa, IGP Sirro anavitaja kuchangia kwa nafasi kubwa ugumu wa usalama wa barabarani, mzizi wa shida kwao ni elimu duni, pia nidhamu duni inayowakosesha utiifu wa sheria pasipo shuruti, kimsingi hawajielewi.

Pia, anataja eneo la miundombinu nalo linabeba mchango mkubwa na kuna baadhi ya maeneo barabarani hayaonyeshi ishara muhimu za kumsaidia dereva, vyote vikichangia katika kusababisha ajali kwa madereva.

Kwa upande wa askari, anakiri wapo baadhi wachache wanakosa uadilifu katika majukumu yao barabarani, hali anayoitaja kuchangia ongezeko la ajali, ingawa anatetea upande wa pili ya walio wengi taratibu na miongozo ya kisheria inatumika.

IGP Sirro anaweka wazi kwamba, kwa askari wanaokiuka maadili ya kazi zao huchukuliwa hatua stahiki.

### MAFANIKIO

Sirro anajivunia kiwango cha mafanikio, kwamba hadi sasa vifo vitokanavyo na ajali barabarani vimepungua na asilimia 25, ingawaje bado viko juu kuliganisha na vinavyohusiana na silaha, hasa bunduki.

Anataja baadhi ya magari ya abiria ya mikoani yanatofautiana maeneo katika mtazamo ama kusafiri usiku au la.

Kwa mujibu wa Sirro, mabasi yaendayo Mwanza na Geita yanasafiri hadi usiku, lakini yaendayo Kigoma yanayazuiwa, kwa sababu kuna mapori njiani yasiyo na usalama kwao.

Akizungumzia polisi kusimamisha gari katikati ya barabara si sahihi na hata kama dereva akisimamishwa, anapaswa kutafuta eneo zuri la kuegessha gari analoendesha.

" Wapo polisi ambao wanasahau weledi wao. Hawatakiwi usimamisha gari katikati (ya barabara)," anatamka na kuingeza kuwa, pia kuna watu anaowaita 'jeuri' kwamba

Anaongeza kuwa pamoja na watu kulalamika kusimamishwa, wale wanaokimbia pindi wakisimamishwa barabarani, inapofika hatua wamekatamwa, ni lazima anaandikiwa kosa kutokana na kukimbia kwake.

"Mara nyingi mtu ambaye anakimbia huwa na makosa ," anasema Sirro, huku akitetea mwenendo wa askari polisi anayejificha na kisa anajitokeza kusimamisha gari, ni mbinu binafsi ya askari kubaini mwenendo halisi wa gari.

Hata hivyo, katika kumtoza dereva faini, anasema sio lazima ifanyike hivyo, ingawa anarejea 'kigezo na masharti kuzingatiwa' kwa kumtaka mkosaji asiwe mkorofi, bali kuomba radhi, hali inayoweza kumwepusha na faini.

Taratibu zinamtaka aliyeandikiwa faini kulipa baada ya wiki moja kwa mujibu wa mashine maalum za risiti tajwa na katika hilo, Sirro anaitolea ufafanuzi ya kuwapo madereva wasiolipa katika muda tajwa, wakiegesha gari nyumbani au kubadilisha namba zake.

Nini kinafanyika kukabili hilo? Sirro ana malelezo:

"Hata gereji au majumbani wanafuatilia ili watu walipe faini."

### UKATILI POLISI

Anasema katika uhusiano wa kijamiii, kuna ukatili wa aina nyingi, akitoa mfano wa mume kumuua mke, mzizi wake ukibebwa na dhana kama vile mume kumfumania mke akiwa na mwanamume mwingine.

Pia, anatoa sura nyingine ya wazee wa kiume kushiriki mapenzi na watoto hata kufika umri miaka tisa, jambo analolisimulia kwao polisi, huwa wanalitatua kupitia nyenzo sheria, pia elimu ya umma, waachane na imani potofu zinazowashika.

Hapo nako kuna kikwazo anachokitaja, kwamba wanajamii wana magumu anayoyataja kujitokeza, hasa katika mikasa ya ndugu au jamaa wa karibu mikasa ya uhaini wa kingono na kubakana, unamalizwa kwa maridhiano ya siri.

Mkuu wa Polisi anataja taratibu zao, zinahusu ama mamlaka za dola hazifahamishwi au inapochukua hatua, bado kesi inazoroteshwa kwa kutoa ushaihidi goigoi, hata shauri hilo mahakamani halifiki mbali kwa kukosa ushahidi wa kuridhisha. Pia, Sirro anataja utoroshaji watoto wenye kesi.

Eneo lingine la jinai linaloshughulikiwa na polisi, lakini ni mwiba kwa afya ya umma, ni kwenye janga la umma kutumia dawa za kulevya, Sirro anasema mbali na hatua za kisheria, pia wanatumia mbadala wa elimu kwa wanafunzi shuleni ili wajihadhari.



Askari wa usalama barabarani, akitetea afya ya umma kazini kwake. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

# Mamia ya wanafunzi wapewa taulo za kike

Na Sabato Kasika

WANAFUNZI 750 wa Tanzania Bara na Visiwani, wamekabidhiwa msaada wa taulo za kike, kwa ajili ya kujisitiri na kuendelea na shughuli zao ikiwamo kuhudhuria masomo bila usumbufu wanapokuwa kwenye hedhi.

Msaada huo ulitolewa na kampuni ya Lavy Beaty Ltd, jana yakiwa ni maadhimisho ya kilele cha Siku ya Hedhi Salama Duniani.

Akizungumzia mgawanyo wa taulo hizo, Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Flaviana Matata, alisema, 480 kati ya hizo zimepelekwa Dodoma na nyingine 270, kwa wanafunzi wa Sekondari ya Kiembe Samaki Islamic Zanzibar.

"Kila sehemu tuna wawakilishi wetu, kule Dodoma taulo zitakabidhiwa kwa wadau wa elimu watazigawa kulingana na mahitaji, kule Zanzibar zimekabidhiwa kwa uongozi wa Kiembe Samaki Islamic Sekondari," alisema Flaviana.

Flaviana alisema, amewahi kuiomba serikali ipunguza ukubwa wa kodi zinazotozwa kwenye taulo hizo na kwamba kama itawezekana, serikali yenyewe ijitolee kuzinunua na kuzigawa bure.

"Suala la hedhi halipaswi kuwa kero kwa mtoto wa kike, lakini imekuwa tofauti kwa watoto wengi wa kike ambao wamekuwa wakipata wasiwasi na kukosa raha wanapokaribia mzunguko wao," alisema.

Alisema, mazingira hayo pia husababisha mtoto wa kike kutojihusisha katika shughuli mbalimbali za jamii kutokana na kukosekana kwa nyenzo za kumsaidia anapokuwa kwenye hedhi.

"Wataalamu wa afya wanasema, mtoto wa kike akipata hedhi salama, anaweza kuondokana na matatizo ya kiafya ikiwamo miwasho, fangasi na magonjwa mengine, hivyo hedhi yenye amani na furaha ni muhimu," alisema.

Meneja wa Marie Stopes Zanzibar, David Mbange, alisema, maadhimisho hayo yanatoa elimu ya kuwa na hedhi salama ambayo inahusisha mtoto wa kike/mwanamke kupata mahitaji yake yote muhimu anapokuwa kwenye hedhi.



Mkuu wa Wilaya ya Mtwara, Dustan Kyobya (katikati), akizungumza na waandishi wa habari jana, wakati wa uzinduzi wa msimu mpya wa mnada wa zao la ufuta mkoani Mtwara. Kushoto ni Meneja Mkuu wa Chama Kikuu cha Ushirika cha Masasi na Mtwara (MAMCU), Potency Rwiza na (wa pili kulia) ni Mkurugenzi wa Mtwara Vijijini, Erica Yegela. **PICHA: ABDALLAH KHAMIS**

# Kunenge awataka watumishi kuondoa kero

**Na Julieth Mkireri,** CHALINZE

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, amewataka watumishi wa Halmashauri ya Chalinze kufanya kazi kwa bidii kutatua kero za wananchi.

Aidha amewasihi madiwani na wananchi kuendelea kumpa ushirikiano Mbunge wa Chalinze Ridhiwani Kikwete, kutokana na kushiriki kutatua vikwazo vya maendeleo vinavyowakabili wananchi.

Kunenge aliyasema hayo alipotembelea halmashauri hiyo kujitambulisha na kusikiliza kero zilizopo kwa wananchi ambazo ziliwasilishwa na madiwani wake.

Alisema ili kufikia malengo ya kuondoa matatizo, ni vizuri kukawa na ushirikiano katika kusukuma gurudumu la maendeleo.

Kunenge alisisitiza nia na dhamira ya uongozi wa Mkoa kuwa ni kuhakikisha pale Halmashauri ya Chalinze walipofikia sasa wanaboresha zaidi, na kwenda kwa kasi kubwa ili iwe halmashauri bora.

Akizungumza baada ya kukabidhi madawati 390 kwa Kunenge kwa ajili ya shule za sekondari 13 za Chalinze, Ridhiwani alisema uhaba wa walimu wa shule za sekondari na upungufu wa madawati bado ni tatizo katika Halmashauri ya Chalinze na kusababisha matokeo ya wanafunzi wanaohitimu kutoridhisha.

Alisema jimbo hilo lina upungufu wa walimu wa masomo ya sayansi, na kwamba wanahitajika walimu 118 kwenye shule za sekondari.

# Wanaowaomba rushwa makandarasi kubanwa

Na Joseph Mwendapole

SERIKALI imewataka makandarasi kuwafichua maofisa wa serikali wanaowaomba rushwa ili wawape upendeleo kwenye zabuni za ujenzi ili hatua kali ziweze kuchukuliwa dhidi yao.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Dk. Leonard Chamuriho, wakati akifungua mkutano wa siku mbili wa mashauriano wa wadau wa sekta ya ujenzi ulioandaliwa na Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB).

Alisema mkandarasi anapopewa mradi kwa kutoa rushwa mara nyingi miradi haikamiliki kwa wakati na wakati mwingine inafanywa kwa viwango vya chini hivyo kuisababishia serikali hasara kubwa kwa kuharibika kwa muda mfupi.

"Sekta ya ujenzi ni eneo ambalo linalalamikiwa sana kwa rushwa hivyo ungeni mkono juhudi za serikali katika kupambana na vitendo vya rushwa kwa sababu kupata zabuni kwa rushwa hakukuendelezi bali kunakudidimiza," alisema Waziri Chamuriho

Vile vile, alisema huu ni wakati mwafaka kwa makandarasi wazalendo kuungana na kutumia fursa zilizopo kutekeleza miradi mikubwa ya ujenzi kwa kuweka ubinafsi pembeni.

Alisema kazi nyingi za ujenzi zinafanywa na makampuni ya nje kutokana na makandarasi wa ndani kukosa uwezo wa mitaji, mitambo ya kutosha na rasilimali watu hivyo kuungana ndiyo itakuwa suluhisho la matatizo yao.

Alisema serikali itatoa tamko hilo mwezi Juni kwenye mkutano wa mashauriano baina ya Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB) na wadau wa sekta ya ujenzi unaotarajiwa kufanyika mkoani Mwanza mwezi Juni.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**Mary Julius Agustino** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S2360/0061** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia Mailisita Sekondari mwaka 2010. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **KIL/MOS/RB/255302/2021.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**SAMWEL NDUGU** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha Sita chenye **index namba S0134-0752** kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia MOSHI SEKONDARI mwaka 2017. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **KAG/BUK/RB/213153/2021.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA UJENZI ,UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

### TANGAZO

Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **JUMAPILI tarehe 30/05/2021** kampuni ya **BENI KUNDAELI MUSHI.** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **DAR ES SALAAM** kuelekea **NJOMBE** kupitia **VIGWAZA.**

1. Gari hilo lenye namba ya usajili na vipimo vyake. **T 398 CJN/ T 450 BKE UREFU 20M UPANA 4.6 M KIMO 5.2M**
2. Gari hilo linatoka **DAR ES SALAAM** kuelekea **NJOMBE** kupitia VIGWAZA .Gari litasafiri muda wa mchana tu(kuanzia saa 12:30 asubuhi mpaka saa 12:00 jioni).

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya TABORA**

**Kituo cha ISEVYA mkoa wa TABORA**

**Usimamizi wa mirathi na.24 2021**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI**

**MAREHEMU WILLIAM ROBERT MGALULA**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA SALMA WILLIAM MGALULA**

**TANGAZO**

(kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi mahakama za mwanzo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo mnamo tarehe 17 mwezi 8 mwaka 2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Imewasilisha leo tarehe 17 mwezi 5 mwaka 2021

**MAHAKAMA YA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA MBEYA**

**SHAURI NO.32/2021**

**GIDA MAIDI::::::::::::::::::::::::::::::::::::::::::::::::::MDAI**

**Dhidi ya**

**BUHOLO MANDALU:::::::::::::::::::::::::::::::::::MDAIWA**

**YAH:KUITWA SHAURINI**

**KWA: BUHOLO MANDALU,**

**Fahamu kwamba GIDA MAIDI amefungua shauri dhidi yako katika baraza hili.**

Shauri limepangwa kutajwa tarehe 17/06/2021 saa 2:30 asubuhi mbele ya Mh.M.Mapunda Mwenyekiti wa Baraza.Unatakiwa kuleta utetezi wa maandishi ndani ya siku 21 tangu tarehe ya wito huu.
Nyaraka zinazohusu shauri hili zinapatikana katika masijala ya Baraza la Ardhi na Nyumba Mbeya.
Unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa wewe mwenyewe au mwakilishi anayeruhusiwa kisheria.Ofisi za baraza zipo ndani ya eneo la Sabasaba Mbeya mjini.
Kumbuka:Usipo hudhuria siku hiyo baraza litatoa amri stahilivu ikiwa ni pamoja na kusikiliza shauri pasipo wewe kuwepo.
Amri hii imetolewa na mkono wangu wa Lakiri/Muhuri wa baraza hili leo tarehe 20/05/2021.

A. Mapunda
MWENYEKITI
20/05/2021.

## KURUDIA TANGAZO LA MNADA

Kwa idhini tuliyopewa na **TUJIJENGE TANZANIA LTD, SEPCO DEBT COLLECTION & AUCTIONEERING CO. LTD** tunarudia tangazo la mnada wa hadhara wa gari la mdaiwa Sugu, mali ya Ndugu **ABDIEL ALPHONCE MSHANA (TOYOTA LEXUS -T 161 AXF)** - Gari lipo katika yard ya Makumbusho.
Lengo ni kufidia/ kupunguza deni la mkopo analodaiwa. Mnada utafanyika Tarehe **07/06/2021,** mahali dhamana ilipo. Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14 akishindwa kulipa 25% hairudishwi.

Gharama za kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.

**Mawasiliano piga: 0715683777/0712670704/0713052578**
**Email: info@sepcoauctioneering.co.tz**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**FREDY JAMES SHALTIEL**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI ZA GARI AINA YA MITSUBISH FUSO ZENYE NAMBA ZA USAJILI **T580 ATQ**
TAARIFA YA POLISI **KAH/TR/RB/553/2019**
NA KADI YA GARI AINA YA MITSUBISH FUSO YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 216 BBF**
KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **KAH/TR /RB/ 553/2019**

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**KINGLION INVESTMENT COMPANY LIMITED**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 146 CFU.**ENGINE NAMBA **KL162FMJK5015105** CHASSIS NAMBA **L7GPCKLY6K1015105.**
YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.
TAARIFA YA POLISI **MBE/MBE/RB/270982/2021**

## TANGAZO LA KUFUNGA KAMPUNI

WAMILIKI WA KAMPUNI YA **DANTAH INDUSTRIES LIMITED,**
NAMBA YA USAJILI **127319**
**TAREHE 30th APRIL 2021.**
WANAPENDA KUUTANGAZIA UMMA KUWA KAMPUNI YAO IMEFILISIKA NA HIVYO KUAMUA KUIFUNGA KWA MUJIBU WA SHERIA YA MAKAMPUNI BRELA.

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI (S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika Mahakama ya Mwanzo MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi NO.155/2021**

**Ombi la HAMISI SHABANI MGAGALA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu RAMADHANI SHABANI MGAGALA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe 24/06/2021 kabla huyo mwambaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 24/05/2021

Sahihi ya Hakimu
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**EAST AFRICA RETAIL CORPORATION** Inatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajil **T633DLQ** aina ya **AUDI AG** yenye Chasis No. **WAUZZZ8EX4A226691 Eng.NO ALTEAA900680.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu kwa kumbukumbu namba **DOD/DOD/RB/RB/125838/2021**

## TANGAZO LA UKUMBI UKUMBI WA HARUSI NI BURE

**PR COMPLEX ILIYOPO SINZA** SHEKILANGO KARIBU NA HOSPITAL YA PALESTINA INATOA **'OFFER'** YA UKUMBI BURE KUANZIA **WATU 600** NA KUENDELEA KUNA **STANDBY GENERATOR NA FULL 'AC' MAPAMBO. CHAKULA , VITI, MEZA, MC NA MZIKI NI JUU YAKO.**

***VINYWAJI VINAPATIKANA UKUMBINI KWA BEI NAFUU. KARIBUNI SANA.***

## TANGAZO LA KUFUNGA KAMPUNI

WAMILIKI WA KAMPUNI YA **IMPERIAL DISTRIBUTORS LIMITED,**
NAMBA YA USAJILI **87116**
**TAREHE 30th APRIL 2021,**
WANAPENDA KUUTANGAZIA UMMA KUWA KAMPUNI YAO IMEFILISIKA NA HIVYO KUAMUA KUIFUNGA KWA MUJIBU WA SHERIA YA MAKAMPUNI YA BRELA.

## OFISI ZA MATANGAZO

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**




TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HADITHI

MWANZONI ilionekana ni fahari. Wazazi kupata mtoto wa kike. Akaja kuwa msichana mzuri aliyeumbwa akaumbika na kutamaniwa na kila mtu, ni sifa kubwa. Wakati mwingine mzazi hupata hata vizawadi vidogo kutoka kwa watu mbalimbali bila kujua kuwa nia ni kutengeneza mazingira kwa binti yao. Kinyume chake mzee Ngoma na mkewe Fatuma wanapata mtoto wa kike Bishada ambaye anaondokea kuwa tishio kwenye kijiji cha Mtakuja kwa urembo wake.

Badala ya kuwa tija na faraha kwa wazazi wake anageuka kuwa balaa. Wazazi wanakuwa hawana amani kutokana na vitisho mbalimbali ikiwemo kuuawa kutoka kwa watu mbalimbali ndani na nje ya kijiji hicho. Inakuwa tafrani. Kijiji hakikaliki. watu wanatafutana. Moto unawaka. Bishada mwenyewe maisha yake yanakuwa hatarini. Fuatilia kisa hiki ambacho kitakuacha mdomo wazi.

# HADITHI

# Aolewe au afe-8

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**

**Na Adam Fungamwango**

"Kukosa yule mwanaume mama nadhani saa hizi ningekuwa nimeshajiua. Nisingekubali kufanyiwa vile halafu niendelee kuwa hai."

"Usiseme hivyo mwanangu, haya yote mambo yanapangwa na Mungu. Kwanza inabidi tumwite ili tumpe shukurani, maana tangu jana kule kwenye Ofisi za Kijiji tulipoachana naye hadi leo hatujamwona."

"Nitaenda kumwita."

"Nani wewe."

"Mimi ndiyo." Bishada alimjibu mama yake huku akitabasamu.

Mama yake alimwangalia usoni binti yake akatabasamu pia.

"Kamwite aje kula chakula cha mchana."

"Kwanza tumchinjie kuku. Yule kuku wangu mmoja, ngoja nimwite mzee Kibedi amchinje kwa ajili ya mgeni."

"Na mpunga ule tuliouanika juzi si upo, tuutwange tumpikie. Na hii itakuwa ni shukrani kubwa kwetu, maana hatuna cha kumpa."

"Kwani yule mgeni ametokea wapi?"

"We mwana we mbona unaniuliza hivyo? Si atakuja mwanangu utamuuliza? Au ukienda kumwita muulize mwenyewe. Wewe ndiyo utatuambia alikotokea."

Kwa mbali, Bishada alianza kuhisi kitu ambacho hakuwahi kuhisi huko nyuma. Hakujua ni nini.

**************************

"Hodi."

"Karibu."

Mwitikiaji badala ya kumsubiri mgeni wake aingie alitoka yeye.


Alifungua mlango. Alichokiona badala ya kumruhusu kupita alisimama mlangoni.

Macho ya Denis yalikutana na yule msichana ambaye alimwokoa jana, asibakwe na kijana mmoja mpuuzi anayejiita Deo.

Alihisi aibu halisi za kike za msichana yule. Ni aibu ambazo zilitokana na kwamba alimkuta ameshatoa nguo zote, kabla ya kumwokoa? Alijiuliza mwenyewe lakini hakupata jibu.

"Unafagia mwenyewe?" Denis aliulizwa swali ambalo hakutegemea. Na muulizaji mwenyewe hakuwa anamwangalia aliyemuuliza.

Ndipo alipojigundua kuwa ana fagio mkononi.




"Ndiyo. Si unajua kuwa nyumba hii ya marehemu mjomba haikuwa inakaliwa na mtu yeyote kwa miezi minne sasa. Ndiyo maana nafanya usafi. Nimelala usiku mmoja tu lakini vumbi la humu ndani nimeamka na mafua." Wote walitabasamu.

"Basi ngoja nikusaidie kufagia." Bishada alimwambia Denis.

Denis bado alishikwa na mshangao. Si kwa sababu ameambiwa asaidiwe kufagia kwa msichana mrembo kama yule. Yeyote ambaye alimsaidia alitegemea kurudishiwa fadhila kama hizo. Alichoshangaa ni msichana huyo kufika kwake.

"Amekuja kufanya nini?" Ndicho alichukuwa anajiuliza.

"We acha tu, kwanza nakaribia kumaliza."

"Hapana. Hata kama umebakisha kidogo. Haiwezekani mimi nipo mwanamke halafu nakuona wewe mwanaume unafagia."

Denis alifikiri kidogo halafu akasema "Haya, basi pita ndani."

Kwa aibu na madaha kidogo, Bishada aliingia ndani na kuanza kufagia.

Denis hakuongea kitu. Alibaki akimtazama Bishada kwa mshangao.

Kwa hakika aligundua kuwa hakumtazama vizuri jana yake.

Uzuri na urembo wake ulionekana kuzidi mara dufu. Akili ya Denis ilienda mbali sana.

Alijikuta kama yeye ndiye mume na anayefagia pale ni mkewe.

Kila akimuangalia aliona bado ni msichana mbichi, anayewaka kama mwezi. Nguo alizovaa ingawa si za gharama sana, pamoja na manukato aliyoyapaka. Nywele ndefu nyeusi, zilimfanya Denis kusimama kama amegandishwa na barafu.

Bishada aligundua hilo. Hakuwa na wasiwasi wowote wa lolote baya kutokea kwa mwanaume huyo.

Kwanza ndiye mwanaume aliyemwokoa kubakwa jana yake. Alionekana ni mtu mwenye heshima na huruma, hivyo hakumtilia shaka.

Kwa kawaida, wanawake wana uwezo mkubwa sana wa kumfahamu mtu, hasa tabia za wanaume kwa muda mfupi tu wanapokutana nao.

"Na nje nako barazani na uwanja mzima wa nyumba ya marehemu mjomba wako, yaani kumekuwa kama jalalani."

"Ndiyo maana nilianza kwanza ndani, halafu mwisho iwe nje."

"Basi usitie shaka, nikimaliza hapa nitakusaidia kufagia na nje." Bishada alisema huku akigung'uta ufagio baada ya kumaliza.

**************************

"Unajua nimekuja hapa nimetumwa na mama." Bishada alisema baada ya kumaliza kufagia uwanja.

Alikuwa amekaa kwenye kigoda, huku Denis akiwa amekaa kwenye kiti. Walikuwa wameketi barazani.

**Denis bado alishikwa na mshangao. Si kwa sababu ameambiwa asaidiwe kufagia kwa msichana mrembo kama yule. Yeyote ambaye alimsaidia alitegemea kurudishiwa fadhila kama hizo. Alichoshangaa ni msichana huyo kufika kwake.**

"Anasemaje mama."

"Kanituma nije nikwite." Bishada alisema huku akiwa ameinamia chini.

"Uniite mimi?"

"Ndiyo."

Denis hakuhisi kama kuna chochote kibaya kwa sababu alimuokoa binti huyo, alitegemea familia au wazazi wake wampe angalau ahsante au shukrani kwa kuzuia unyama dhidi ya binti yao.

"Samahani nikuulize kitu?" Sauti ya Denis ilikuwa tulivu.

"Uliza tu."

"Natanguliza kwanza samahani kwa sababu sitaki kukukumbusha kilichotokea jana. Lakini naomba tu uniambie kwa nini yule jamaa aliamua kufanya hivyo? Na kuna nini kwenye kijiji hiki, maana kuna maneno niliyasikia wakati namkabidhi pale kwa Mwenyekiti wa Kijiji yalikuwa yanaongelewa."

Bila ya samahani. Bila ya kuacha neno lolote. Bishada alimhadithia Denis kila kitu kilichotendeka kwenye kijiji hicho hadi kufikia pale alipomkuta.

"Kwa hiyo mna wiki moja tu ya kukaa hapa?" Ndiyo.

"Na wewe bado hujaamua kukubali barua yoyote ya uchumba?"

Bishada alisita kwanza. Kwa mara ya kwanza akamwangalia mgeni yule kwa sekunde nyingi kuliko zote tangu afike pale akajibu "Ndiyo". Alipojibu akamwangalia tena.

"Kwa wewe sitokubali uondoke." Jibu hilo lilionekana kumfurahisha Bishada. Alitoa tabasamu pana.

"Kwa nini?" Aliuliza.

"Sijamzoea yeyote kwenye kijiji hiki zaidi yako. Ukiondoka nitabaki na nani?"

"Mbona wewe mwenyewe unakaa kwa muda tu kwa ajili ya mashamba ya mjomba wako, si utaondoka na wewe?"

"Nitaondoka na wewe. Au na mimi utanitosa?" Aliuliza kwa utani.

Bishada alitabasamu na uso akauelekeza kuangalia chini."

"Haya mama, twende nyumbani kwenu, sijui umenipikia nini."

Bishada aligeuza kichwa kwa mbwembwe. "Wali kuku." Aliongea kwa sauti ya chini ya kunong'oneza.

"Muongo."

"Kweli tena."

"Haya kwenu mimi sikujui. kwa hiyo nishike mkono."

Bishada aliangua kicheko kikali ambacho kilitoka bila hiyari yake. Akamshika mkono Denis.

"Haya twende." Wote wawili walijikuta wakiangua vicheko vya furaha.

**ITANEDELEA JUMAMOSI**

## HABARI MICHEZO

# DE GEA KUBADILISHANA NA OBLAK




**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United imepanga kumtumia golikipa wake, David de Gea kama chambo ili kumpata mlinda mlango wa Atletico Madrid, Jan Oblak, kwa mujibu wa The Sun.

De Gea ametumia mwongo mmoja akiwa na klabu hiyo, lakini kiwango chake kimekuwa sio cha kuvutia katika miaka ya hivi karibuni.

Na sasa United inataka kumtumia De Gea ili kumpata Oblak ili kumaliza tatizo lao la mlinda mlango.

Majaliwa ya De Gea yamekuwa na sintofahamu tangu Dean Henderson aliposaini mkataba wa muda mrefu na United.

De Gea ambaye ni mchezaji wa kimataifa wa Hispania, alijiunga na Atletico mwaka 2011.

Nyota huyo kwa muda mrefu amekuwa akihusishwa na mpango wa kurudi Hispania, huku Real Madrid ikitajwa kumwania.

Hata hivyo, miamba wa Ligi Kuu Ufaransa, PSG pia imekuwa ikihusishwa na mpango wa kuwania saini yake.

# Kante, Mendy fiti kucheza fainali Uefa

**LISBON,** Ureno

KIUNGO wa Chelsea, N'golo Kante yupo fiti na sasa amerejea mazoezini tayari kuwavaa Manchester City katika mechi ya fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya itakayochezwa leo Jumamosi.

Chelsea itakutana na City katika fainali hiyo itakayopigwa nchini Ureno, ambapo kulikuwa na tetesi kuwa Kante anaweza akakosa mchezo huo baada ya kupata majeruhi kwenye mechi zilizopita.

Kwa upande mwingine pia, kipa namba moja wa timu hiyo, Eduardo Mendy amerejea mazoezini kuungana na wenzake katika maandalizi ya mechi hiyo ya fainali.

Kante amekuwa na mchango mkubwa kwenye mechi za Chelsea katika michuano hii ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na mashabiki wengi wa Chelsea walikuwa wanahofia kukosekana kwa mchezaji huyo.

Mendy pia amemaliza Ligi Kuu England akiwa kipa wa pili ambaye hajaruhusu nyavu zake kutikiswa kwa mechi nyingi.






# Allegri kumrithi Pirlo Juventus

**TURIN,** Italia

JUVENTUS itaachana na Kocha wake Mkuu, Andrea Pirlo na nafasi yake itachukuliwa na Massimiliano Allegri, kwa mujibu wa ripoti kutoka nchini Italia.

Pirlo alisaini mkataba wa miaka miwili akichukua nafasi ya Maurizio Sarri hapo Bianconeri Agosti mwaka jana, lakini kocha huyo mwenye umri wa miaka 42 ameshindwa kufikia matarajio.

Kiungo huyo wa zamani wa Italia alishindwa kuiwezesha Juve kutetea taji la Ligi Kuu Italia ambalo ililitwaa mara tisa mfululizo.

Mazeti ya Italia, La Gazzetta dello Sport na Corriere dello Sport yote yameripoti tayari makubaliano yamefikiwa kati ya Juve na Allegri.

Juventus imefuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa msimu wa 2021-22 baada ya kumaliza nafasi ya nne kwenye msimamo huku, Inter ikishinda taji la Ligi Kuu Italia.

# Kamari yamweka matatani Zlatan

**MILAN,** Italia

MCHEZAJI mkongwe wa AC Milan, Zlatan Ibrahimovic amejikuta kwenye hatia na kupigwa faini ya euro 50,000 baada ya kubainika alikuwa na hisa kwenye kampuni moja ya kamari.

Baada ya uchunguzi uliofanywa na Shirikisho la Soka Ulaya (UEFA), imebainika kuwa mchezaji huyo wa Serie A anamiliki asilimia 10 ya hisa katika kampuni ya kamari ya Berthard, hivyo kosa hilo linavunja moja kwa moja sheria za kinidhamu za UEFA.

"Mwenyekiti wa UEFA ameamua kumpiga faini ya euro 50,000 kwa Zlatan Ibrahimovic kwa kuvunja kifungu namba 12(2)b cha kitengo cha nidhamu yaani kuwa uhusiano wa kifedha na kampuni ya kubashiri."

"Mwenyekiti wa UEFA ameamuru pia kuwa Ibrahimovic ajiondoe kwenye ushiriki wa kampuni tajwa.

"Pia AC Milan imeonywa na kupigwa faini ya euro 25,000 kwa kuruhusu kuwa na mchezaji anayejihusisha na kumiliki hisa katika kampuni ya kubashiri."





# ODEGAARD NJIAPANDA MADRID

**MADRID,** Hispania

REAL Madrid wanaripotiwa kuwa bado hawajafanya maamuzi juu ya hatima ya nyota wao, Martin Odegaard.

Nahodha huyu wa Norway amekuwa na msimu wake mzuri wa mkopo pale Arsenal, lakini Real Madrid wamekuwa wakiripotiwa kuwa wanataka kumjumuisha kwenye mipango ya kikosi chao cha msimu ujao 2021-22.

Hata hivyo, kwa mujibu wa AS, kuna mgogoro ndani ya mamlaka za Real ikiwa Odegaard anatakiwa auzwe au asalie klabuni hapo kuelekea msimu mpya.

Ripoti zaidi zinasema kwa kuzingatia hali ya kiuchumi ya Real Madrid, uamuzi wa kumuuza nyota huyo ni jambo linalotarajiwa zaidi, lakini nyota huyu anaonekana kuwa sehemu muhimu ya siku zijazo za Real Madrid, akishirikiana na Federico Valverde.

Odegaard amefunga mabao mawili, na kutoa usaidizi wa mabao mbili zaidi kwa ajili ya Arsenal kwa michuano yote kwa kipindi alichokuwapo Arsenal kwa mkopo.

# Konate, Liverpool kimeeleweka

**LIVERPOOL,** England

MLINZI wa RB Leipzig, Ibrahima Konate anatarajiwa kuwa usajili wa kwanza wa Liverpool katika majira haya ya joto, taarifa imethibitishwa mapema wiki hii.

Mchezaji huyo atajiunga na Liverpool kwa mkataba wa kudumu huku taarifa zikisema tayari alikuwa na makubaliano na Majogoo hao tangu Aprili, mwaka huu.

Beki huyo anatarajiwa kusaini mkataba wa miaka mitano na Liverpool ambao utamalizika ifikapo Juni, mwaka 2026 huku tayari kukiwa na makubaliano binafsi.

Mkataba huo utasainiwa na RB Leipzig katika siku zijazo, Konaté anataka tu kujiunga na Liverpool na kifungu cha kutolewa kitakuwa ufunguo wa kukamilisha makubaliano katika siku zijazo.

Liverpool hawajaamua rasmi bado juu ya chaguo la kumnunua la Ozan Kabak, lakini inaelezewa hawataweza kumsajili beki huyo kwa mkataba wa kudumu baada ya kumalizana na Konate.



HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MESSI, BARCELONA SASA KIMEELEWEKA

## Ni baada ya bosi na baba wa mshambuliaji huyo kufanya kikao chanya kuhusu hatima ya...

**BARCELONA,** Hispania

MAZUNGUMZO kati ya Barcelona na Lionel Messi juu ya mkataba mpya yanaendelea vizuri sana, huku Rais Joan Laporta akikutana na baba mzazi wa mchezaji huyo ambaye ni wakala wake, kwa mujibu wa wa ESPN.

**ESPN imethibitisha kupitia Catalan TV3 kwamba, Messi anaelekea kufikia makubaliano na Barca, baada ya Laporta kufanya kikao cha muda mrefu na Jorge Messi (baba mzazi wa nyota huyo).**

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, Barca ipo tayari kufikia matakwa ya Messi ili aweze kuendelea kubakia hapo Camp Nou kwa misimu mingine zaidi.

Mkutano huo "ulikuwa chanya sana," na chanzo kimoja kimeiambia ESPN, lakini Messi, ambaye mkataba wake unamalizika Juni 30, anataka kujua mpango wa maendeleo wa klabu hiyo kabla ya kufanya uamuzi.

ESPN iliripoti mwezi uliopita kwamba, rais wa Barca, Laporta alipanga kumpa Messi ofa ya mkataba wa miaka miwili huku kukiwa na kipengele cha kuongeza mwaka mmoja.

Kama Messi atafikia makubaliano na Barca maana yake mpango wa kwenda kucheza Ligi Kuu Marekani (MSL), utakuwa umefikia mwisho.

Messi alibainisha Desemba kwamba "matumaini yangu ni kufuata mataji na kutapa uzoefu wa soka la Marekani" na wazo hilo linaonekana bado kuwa kwenye akili yake.

Kwa mujibu wa TV3, ofa ya Laporta kwa sasa ni ya miaka mitano kwa nyota huyo wa kimataifa wa Argentina ili amalizie soka lake hapo Barcelona.

Messi kwa sasa mshahara wake ni euro milioni 70 kwa msimu mmoja, na inaonekana kwamba unaweza kuongezwa zaidi.

## ZISIKUPITE

### CONTE KUTUA SPURS

KOCHA wa zamani wa Chelsea, Antonio Conte, ambaye ameachana na klabu ya Inter Milan Jumatano wiki hii anataka kujiunga na Tottenham Hotspur. ***(Guardian)***

### ZIDANE ATAJWA EPL

INGAWA Tottenham Hotspur, inaangalia pia uwezekano wa kumchukua kocha aliyeondoka Real Madrid, Zinedine Zidane. ***(Telegraph)***

### SOLSKJAER, UNITED SAFI

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer anajiandaa kusaini mkataba mpya wa miaka mitatu na klabu hiyo yenye maskani yake katika dimba la Old Trafford. ***(Telegraph - subscription required)***

### UNITED KUSAJILI WATATU

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunna Solskjaer anapanga kusajili wachezaji watatu kama kipaumbele chake katika dirisha la usajili la majira haya ya joto. Wachezaji hao ni mlinzi wa Villarreal, Pau Torres (24), pamoja kiungo wa West Ham, Declan Rice, winga wa Borussia Dortmund, Jadon Sancho na mshambuliaji wa Tottenham, Harry Kane (27). ***(Guardian)***

### PIRLO AKALIA KUTI KAVU

KLABU ya Juventus inatarajiwa kumfuta kazi kocha wake, Andrea Pirlo na kumrejesha kocha wao wa zamani, Massimiliano Allegri. ***(Guardian)***

### MADRID YAMTAKA ALLEGRI

KLABU ya Real Madrid inampigia hesabu Massimiliano Allegri ili kuchukua nafasi ya Zinedine Zidane, ambaye amejiuzulu kuinoa klabu hiyo Alhamisi.***(Mail)***

### POCHETTINO SOKONI

KLABU ya Real Madrid sasa wanatarajiwa kuhamishia nguvu zao katika kumsaka kocha wa PSG Paris St-Germain, Mauricio Pochettino. ***(Goal)***

### INZAGHI ATUA INTER

SIMONE Inzaghi anatarajiwa kutangazwa kuwa kocha wa Inter Milan baada ya kuachana na klabu ya Lazio. ***(Athletic - subscription required)***

### XHAKA ANUKIA ROMA

KOCHA wa zamani wa Tottenham Hotspur, Jose Mourinho anamtaka kiungo wa Timu ya Taifa ya Uswisi na Arsenal, Granit Xhaka mwenye umri wa miaka 28. ***(Sky Italy, via Metro)***

### ARSENAL KUTAJIRIKA

ARSENAL wanatazamiwa kutaka kulipwa dau la pauni milioni 21.5 kwa ajili ya Granit Xhaka, AS Roma wanaamini watalipa kitita kisichozidi pauni milioni 10. ***(Sky Sports)***

### KOEMAN KUIKAMUA BARCA

KUMFUKUZA kazi kocha Ronald Koeman kutawagharimu Barcelona takribani pauni milioni 12. ***(RAC1)***

HABARI MICHEZO

## Mtibwa Sugar yasaka michezo

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Mtibwa Sugar, Mohammed Badru, amesema anahitaji kupata mechi mbili za kirafiki katika kipindi hiki ambacho Ligi Kuu Tanzania Bara imesimama ili kukiimarisha kikosi chake kuelekea mechi za hatua ya lala salama.

Mtibwa Sugar itashuka dimbani ugenini Juni 17, mwaka huu, dhidi ya Mwadui FC ya Shinyanga ambayo kihesabu imeshashuka daraja.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam, Badru alisema mapumziko aliyowapa wachezaji wake yameisha na jana walitarajia kuingia kambini Morogoro kuendelea na maandalizi ya mechi nne zilizobakia.

Badru alisema muda wa wiki tatu ambao watakaa bila kucheza mechi ya ligi, anatamani kupata michezo ya kirafiki ambayo itamsaidia kurekebisha mapungufu ya kikosi chake na hatimaye kumaliza msimu wakiwa imara.

"Tunakaa muda mrefu bila ya kucheza, pia hatuko sehemu salama katika msimamo, nimelazimika kutafuta mechi mbili za ushindani, ningependa kucheza na timu ambazo tuko nao kwenye ligi ili kuona mapungufu yetu na kuyafanyika kazi kabla ya kurejea katika mechi rasmi," alisema Badru.

Mtibwa Sugar imebakiza mechi dhidi ya Mwadui FC (Kambarage, Shinyanga), KMC FC (Uhuru- Dar es Salaam) na Dodoma jiji FC na baadaye watamaliza msimu huu dhidi ya JKT Tanzania kwenye Uwanja wa Jamhuri, jijini Dodoma.

## Kagera yatangaza vita Ligi Kuu Bara

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Kagera Sugar imesema mechi nne zilizosalia za timu yao katika msimu huu wa Ligi Kuu Tanzania Bara unaoelekea ukingoni watacheza kufa au kupona, imeelezwa.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Francis Baraza amesema anajua ugumu wa mechi hizo zinazofuata, lakini lazima wapambane ili kuhakikisha wanabaki kwenye ligi hiyo ya juu nchini.

"Tunaendelea na maandalizi. Tumebakisha mechi nne ili tumalize ligi, ni lazima tupambane kuhakikisha tunabaki. Uwezo huo upo na tumejipanga kwa hilo," alisema Baraza.

Kocha huyo ambaye ni raia wa Kenya aliichukua Kagera Sugar Machi, mwaka huu, baada ya kufanya vyema kwenye kikosi cha Biashara United kwa misimu miwili. Hata hivyo, alijiunga na Kagera Sugar ikiwa kwenye hali mbaya, ikiwa imemtimua kocha wake, Mecky Maxime.

Mpaka sasa iko kwenye nafasi ya 13, ikiwa na pointi 33 kwa michezo 30 ambayo imeshacheza mpaka sasa na mechi zake zilizobaki ni dhidi ya Polisi Tanzania, Prisons, Ihefu na Coastal Union.

# KMKM, POLISI HATUMWI MTOTO LIGI KUU ZANZIBAR

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

VITA ya kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar inatarajia kuendelea tena leo kwa timu za 'Maafande' KMKM kuwakaribisha Polisi kwenye Uwanja wa Amaan Visiwani hapa.

**KMKM inahitaji ishinde michezo miwili au mmoja ili kutangazwa mabingwa wa ligi hiyo endapo wapinzani katika mbio hizo watapoteza mchezo mmoja.**

Kwa hali hiyo hatima ya ubingwa wa KMKM upo mikononi mwa Polisi ambayo pia inapambana kutaka kujinusuru na janga la kushuka daraja.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa KMKM, Ame Msimu, alisema mchezo huo utakuwa mgumu na wenye ushindani kwa sababu kila timu itashuka uwanjani ikiwa na lengo lake.

Msimu alisema amewaandaa wachezaji wake kupambana kuhakikisha wanapata matokeo mazuri ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kutawazwa mabingwa wapya kwa msimu huu wa 2020/21.

"Haitakuwa mechi ndogo, tunatarajia ushindani kuliko tuliokutana nao kwenye michezo iliyopita, mechi ya kesho (leo), kila timu ina malengo yake, sisi tunataka ubingwa na wapinzani wetu wao wanataka kubaki katika Ligi Kuu," alisema Msimu.


Aliongeza kwa upande wake anaufananisha mchezo huo na fainali kwa sababu wakifanikiwa kupata alama tatu basi tayari safari yao ya kutangazwa mabingwa wa msimu huu itakuwa imekaribia.

"Tumejiandaa kupata alama tatu, kikosi chetu kipo tayari kwa ajili ya kupambana, wachezaji wote hivi sasa wanasubiri mchezo huo ambapo kwetu ni kama nusu fainali au fainali, pia itategemea na matokeo ya wapinzani wetu, tunaomba dua lengo litimie na wachezaji wazingatie yote tuliowaelekeza sisi walimu wao," Msimu alisema.

Naye Kocha Mkuu wa Polisi, Yusuph Sape, alisema hautakuwa mchezo rahisi kwa kuwa kila timu inahitaji kupata alama tatu ambazo zitawapa faida kwenye mbio zao.

"Sisi tunahitaji alama tatu ili tujihakikishie kubaki katika Ligi Kuu, wapinzani wetu wanahitaji pointi tatu ili wajirahisishie zaidi mbio za ubingwa msimu huu, hivyo kwa kifupi utakuwa mchezo wa vita ya kupambana kila mmoja lengo lake litimie," alisema Sape.

Mechi nyingine ya ligi hiyo itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Mau A itakuwa ni kati ya Zimamoto dhidi ya KVZ ambazo nazo ziko katika nafasi ya kutwaa ubingwa.



Mwakilishi wa Kampuni ya Silent Ocean, Mohamed Kimilagwa (kushoto), akimkabidhi mfano wa tiketi ya ndege mwanariadha, Augostino Sule wa jijini Arusha kwa ajili ya kwenda kushiriki mbio za Langa zitakazofanyika Afrika Kusini, ili kusaka tiketi kushiriki mashindano ya Olimpiki yatakayofanyika Agosti mwaka huu, nchini Japan. Katikati ni Mratibu wa Mr.UK Marathon, Nelson Mrashani. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Twanga Pepeta kuzindua mpya leo

**Na Mwandishi Wetu**

BENDI ya muziki wa dansi ya African Stars maarufu Twanga Pepeta inatarajia kuzindua albamu yake ya 14 katika onyesho litakalofanyika leo kwenye Ukumbi wa Club Brake Point uliopo kwenye Kijiji Cha Makumbusho, Kijitonyama jijini Dar es Salaam.

Uzinduzi huo utaambatana na mchakato wa kutoa tuzo kwa wanamuziki mbalimbali waliotukuka wa hapa nchini, Mwenyekiti wa bendi hiyo, Asha Baraka amesema.

Baraka alisema mbali ya kutambulisha nyimbo mpya zilizoko katika albamu hiyo, pia watapiga nyimbo mbalimbali za albamu za zamani ili kuwakumbusha mashabiki wao enzi za nyimbo hizo.

Alisema jina la albamu hiyo litapatikana baada ya kupigia kura nyimbo zilizomo katika onyesho hilo.

Alizitaja baadhi ya nyimbo zinazounda albamu hiyo ni pamoja na Twanga Mbele, Rekebisha, Povu, Penzi Sigara Kali, Push to Star na Ingekuwa na tayari wameanza maandalizi ya kutengeneza video za nyimbo.

"Ni muda mrefu hatujafanya uzinduzi wa albamu za bendi na hii ilitokana na sababu mbalimbali, tumeamua kuja kivingine na tutafanya uzinduzi wa kihistoria," alisema Baraka.

Kuhusiana na tuzo za wanamuziki waliotukuka, Baraka alisema wameamua kutoa tuzo hizo kwa kuthamini mchango mkubwa uliotolewa na wadau hao katika sekta ya muziki.

Michezo

Jumamosi Mei 29, 2021

Nipashe



Messi, Barcelona kimeeleweka UKURASA 22



Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Kim Poulsen (kulia), akitangaza kikosi cha timu hiyo kitakachoingia kambini kujiandaa na mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya Malawi itakayochezwa Juni 13, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Ofisa Habari wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), Clifford Ndimbo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Nabi awatafutia kasi nyota Yanga

**Na Saada Akida**

WAKATI Kocha Mkuu wa Yanga, Nesreddine Nabi akiwapa mapumziko mafupi wachezaji wake katika kipindi hiki ambacho Ligi Kuu Bara imesimama kupisha kalenda ya kimataifa, kikosi hicho kinatarajia kucheza mechi moja ya kirafiki ili kujiimarisha.

Taarifa kutoka ndani ya Yanga zinasema mechi hiyo ya kirafiki itakuwa dhidi ya Mtibwa Sugar na imepangwa kufanyika kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Nabi alisema baada ya kutinga hatua ya nusu fainali ya mashindano ya Kombe la FA kwa kuifunga Mwadui FC mabao 2-0, amewapa mapumziko ya muda mfupi wachezaji wake huku akiwapa maelekezo maalumu ya kujitunza.

"Kwa sasa hatutakuwa na mchezo wowote, nimeona bora kuwapa mapumziko ya wiki moja wachezaji wangu, na baada ya siku hizo kumalizika tutarejea kwa ajili ya maandalizi ya mechi dhidi ya Ruvu Shooting, tumetoka katika mechi ngumu ya FA na tunashukuru tumeshinda," alisema Nabi.

Kocha huyo alisema anaamini mchezo huo utawasaidia wachezaji wake ambao hawajaitwa kwenye timu za taifa kujijenga na kuwa tayari kupambana katika mechi zilizobakia za Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya Kombe la FA.

Aliongeza anahitaji kuona wachezaji wote wako tayari kuisaidia timu hiyo kufikia malengo ya kukata tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa katika msimu ujao.

Yanga yenye pointi 61 sawa na vinara Simba wako katika nafasi ya pili kwenye msimamo wa ligi hiyo baada ya kucheza mechi 29.

# Simba, Namungo hesabu hadharani

## Makocha wa timu hizo watambia uzoefu waliopata katika michuano ya CAF, lakini...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

NI pointi tatu tu! Neno ambalo limetawala kwa makocha wa timu mbili, Simba na Namungo, kuelekea mchezo wa kiporo cha Ligi Kuu Tanzania Bara utakaowakutanisha leo kwenye Uwanja wa Majaliwa ulioko Ruangwa mkoani Lindi.

**Timu hizo mbili hazijakutana katika msimu huu kutokana na majukumu ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika pamoja na Kombe la Shirikisho Afrika ambayo walikuwa wakichuana na klabu za nje ya Tanzania.**

Akizungumza na gazeti hili jana kabla ya kuelekea Lindi, Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes, alisema baada ya kuondolewa kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, sasa wamerejea 'kamili' kwenye Ligi Kuu Bara na leo wataingia uwanjani kusaka ushindi tu.

Gomes alisema wanahitaji kuondoka na pointi tatu muhimu katika mechi ya leo ili kufikia malengo ya kutwaa ubingwa na kukata tiketi ya kushiriki tena michuano ya kimataifa ya msimu ujao.

Kocha huyo alisema anatarajia mchezo huo utakuwa mgumu na wenye ushindani mkubwa kwa sababu wao wanahitaji matokeo chanya ili kufikia malengo yao lakini wapinzani wao wanahitaji alama hizo ili kuendelea kujiweka katika nafasi nzuri.

"Malengo yetu ni kushinda kila mchezo ulioko mbele yetu ili kutetea taji letu, kikosi changu kiko fiti na tumejipanga kuanza kutafuta pointi muhimu dhidi ya Namungo FC, nina matarajio makubwa katika mechi hiyo, tumeshafanyia kazi mapungufu yaliyojitokeza katika mchezo wetu dhidi ya Dodoma Jiji, sasa tunaenda kutafuta pointi ugenini ili kufikia malengo yetu," alisema Gomes.

Aliongeza wanawaheshimu Namungo FC na hawataingia kwa kuwabeza, kwa sababu ni timu yenye wachezaji wazuri ambao wanaweza kupata matokeo mazuri kama ilivyo kwa kikosi chake ambacho kinahitaji kujiimarisha kileleni mwa msimamo wa ligi.

Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu, alisema wachezaji wote wako kwenye hali nzuri na lengo lao ni lile la kutetea ubingwa, hivyo kusaka ushindi dhidi ya Namungo FC ndio kipaumbele chao.

Kocha Mkuu wa Namungo FC, Hemed Morocco, alisema wamejipanga vizuri na tayari aliyafanyia kazi mapungufu yao ikiwamo safu ya ushambuliaji ili kuhakikisha wanazibakisha pointi tatu hapo nyumbani kwao.

"Ni mechi ngumu kwa pande zote mbili, kwetu tunahitaji kupata pointi muhimu ili kijiweka sawa katika malengo yetu ya kuendelea kubaki kwenye ligi, pia wenzetu Simba wako vizuri kutokana na ubora ambao wameonyesha katika Ligi ya Mabingwa na pia wanahitaji kujiimarisha katika nafasi waliyopo sasa, (kuongoza ligi)," alisema Morocco.

Naye Ofisa Habari wa Namungo, Kindamba Namlia, aliliambia gazeti hili wanatarajia mechi itakuwa ngumu kutokana na ubora wa Simba hivi sasa, lakini wao wamejipanga sawa sawa kuhakikisha 'mnyama anachinjwa'.

"Kusema kweli Simba ni timu nzuri hapa Tanzania, na hivi karibuni tu imetoka kucheza mechi za kimataifa za Afrika, na wamecheza vizuri, lakini na sisi pia tumeshiriki michuano ya kimataifa pia. Kwa hiyo tunajua jinsi gani ya kucheza nao, kwa kufuata maelekezo ya kocha wetu, tunaamini tutapata ushindi katika mechi hii," Kindamba alisema.

Simba ndio mabingwa watetezi na vinara wa ligi hiyo wakijikusanyia pointi 61 baada ya kucheza michezo 25 wakati Namungo FC inashika nafasi ya nane ikiwa na pointi 40 na imeshuka dimbani mara 28.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 9

9 770856 541002 >